# Nipashe

Jumamosi Juni 19, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580611

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Zuchu asakwa, Wimbo wake wateteresha ndoa**

UKURASA 11

**Samia** atangaza bendera nusu mlingoti siku saba kumwomboleza Kaunda

UKURASA 2



**Nape** awasha moto mfumo wa uagizaji mafuta kutoka nje

UKURASA 3




# Serikali yatoa msimamo kuhusu chanjo ya corona

UKURASA 2


## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**SERIKALI YAANZA MCHAKATO KUFUMUA MTAALA WA ELIMU**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ametangaza rasmi...

**UKURASA WA 4**

**RC AZIPIGA MARUFUKU KAMPUNI UNUNUZI WA PAMBA**

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amepiga marufuku kampuni mbili zilizopewa vibali vya...

**UKURASA WA 5**

**WAZIRI AIBUA STAILI MPYA YA KUDAI KODI**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, ameibuka na staili...




Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (kushoto), akiaga mwili wa aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Prof. Mwesiga Baregu, KKKT Usharika wa Kunduchi, Dar es Salaam jana na baadaye ulisafirishwa kwenda Bukoba kwa maziko. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Usiyoyajua kuhusu Profesa Baregu

UKURASA 7



Wananchi kutoka katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, wakiwa nje ya geti la kuingia katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha jana, wakisubiri kusikiliza kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Kishindo wananchi Sabaya kortini

UKURASA 3


**MICHEZO** **KIPA METACHA ASIMAMISHWA YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Samia amliilia Kaunda, bendera nusu mlingoti

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametangaza siku saba za maombolezo ya kitaifa kutokana na Rais wa kwanza wa Zambia na mwasisi wa taifa hilo, Dk. Kenneth Kaunda, kilichotokea juzi Lusaka, nchini humo.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilieleza kuwa katika kipindi hicho cha maombolezo, bendera zote zitapepea nusu mlingoti.


Pia kutokana na kifo hicho, taarifa ilieleza kuwa Rais Samia ametuma salamu za rambirambi kwa Rais wa Zambia, Edgar Lungu, familia ya marehemu na wananchi wote wa Zambia kwa kumpoteza kiongozi huyo.

Katika salamu hizo, Rais Samia amemtaja Hayati Dk. Kaunda kuwa miongoni mwa viongozi mahiri na jasiri kuwahi kutokea barani Afrika.

Alisema wakati wa uhai wake, alitoa mchango mkubwa kwenye harakati za ukombozi wa Afrika kwa kushirikiana na viongozi wengine, akiwamo Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Vilevile, Hayati Dk. Kaunda alikuwa miongoni mwa waanzilishi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Rais alisema Tanzania itamkumbuka Hayati Dk. Kaunda kwa mchango wake katika kukuza uhusiano na ushirikiano kati yake na Zambia, ambao uliwezesha kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwamo Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Bomba la Kusafirisha Mafuta (TAZAMA).

**Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema Peponi.**




Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, akipokea mfano wa hundi ya Sh. bilioni 21.8 kutoka kwa viongozi wa Benki ya NMB akiwemo Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Edwin Mhede (wa pili kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna (kulia), ambazo ni gawio la benki hiyo kwa serikali, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatoa msimamo chanjo corona

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kukiwa na taarifa kuwa Tanzania imeandika barua kwenda Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, kuomba kuingizwa kwenye mpango wa chanjo za corona zitakazoingia nchini wiki mbili zijazo, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amesema bado suala hilo liko ngazi ya Baraza la Mawaziri.

Akihojiwa na vyombo mbalimbali vya habari vya kitaifa na kimataifa juzi, Msigwa alisema Rais aliunda kamati ya wataalam ambayo ilishafanya kazi na kuwasilisha ripoti serikalini, hivyo hatua inayofuata kupita kwenye mchakato wa Baraza la Mawaziri ndiyo msimamo rasmi utatoka.

"Nawaomba Watanzania tuwe na subira. Tusubiri serikali itakapokuwa tayari itazungumza hayo yote kama kuna chanjo au hakuna hayo yote, au kuna hiki kitafanyika Watanzania tuendaje, hayo yatafanyika baada ya kufanya uchambuzi wa taarifa ya wataalam," alisema.

Msigwa ambaye alisema hajaiona wala kusikia taarifa ya WHO, alisema: "Taarifa tunayopenda Watanzania waipate ni kuwa kwa sasa serikali inachakata mapendekezo ya wataalam yaliyowasilishwa na kamati ikiwamo kulihusisha baraza la mawaziri. Msimamo wa serikali kwa suala hilo (chanjo) haujatoka, nawaomba Watanzania watulie."

Alisema serikali utafanya uamuzi kwa kuzingatia mazingira ya mahitaji ya nchi kwenye suala hilo wakati utakapofika.

Kwa mujibu wa Msigwa, serikali itatoa melekezo kwenye taarifa ya serikali baada ya Bazara la Mawaziri kuchakata taarifa hiyo na ndipo itajulikana kama itawasili lini na kwamba hakuna kitakachofichwa.

"Kwa sasa hakuna uamuzi wowote uliofanywa na serikali juu ya suala hilo.. tusubiri itawekwa wazi baada ya serikali kuchakata taarifa ya kamati," alisisitiza Msigwa.

Juzi, Mkuu wa WHO Kanda ya Afrika, Dk. Matshidiso Moeti, akizungumza na waandishi wa habari alisema wamepokea taarifa rasmi kutoka Tanzania ikiomba kujiunga kwenye mpango wa COVAX unaolenga kuhakikisha nchi maskini kote duniani zinapata mgawo sawa wa chanjo.

Moja ya mapendekezo ya kamati iliyotolewa mwezi uliopita ni chanjo ya corona ni muhimu lakini iwe ni hiari.

# Serikali yaanza mchakato kufumua mtaala wa elimu

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ametangaza rasmi serikali kufanya mabadiliko ya mtaala wa elimu kwa mara ya sita.

Amesema mabadiliko hayo yanalenga kuondoa mtazamo hasi kwenye jamii kwamba manufaa chanya ya elimu kwa wahitimu yanachukua muda mrefu.

Prof. Ndalichako amesema serikali itazingatia maoni yatakayotolewa na wadau kuhusu uboreshaji mitaala ya elimu ili kujenga ujuzi, maarifa na stadi za kazi na kwamba Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) itaboresha mitaala ngazi ya elimu msingi, ikizingatia maarifa kumudu mazingira yaliyopo na ushindani wa soko la ajira.

Profesa Ndalichako alitoa kauli hiyo jana mkoani Dar es Salaam kwenye mkutano wa wadau wa elimu uliolenga kutoa maoni namna ya kuboresha elimu kuanzia ngazi ya shule za msingi, sekondari na chuo kikuu.

Alisema Tanzania inahitajika wahitimu wabunifu watakaoleta ushindani katika uchumi wa viwanda.

"Kila mara mmekuwa mkisema tunakaa na mtoto wako miaka saba au zaidi lakini akirudi hajui chochote, sasa serikali yenu ya awamu ya sita imesikia kilio chenu.

"Wahitimu wanamaliza wakisubiri matangazo ya kazi, ajira, mtaala ujikite kwenye maeneo yapi ili waweze kujitegemea? Hili litazingatiwa," alisema.

Profesa Ndalichako alisema mkutano ni sehemu ya maelekezo ya Rais Samia kuhusu uboreshwaji wa elimu kwa kufanya mapitio ya mitaala na kwamba wizara iliona umuhimu wa ushirikishwaji wa wadau hao ili kila Mtanzania atoe maoni namna elimu inavyotakiwa iwe kwa watoto wao.

"Nyumba bora hujengwa katika msingi ulio imara kwa sababu hii itasaidia kujenga msingi bora na kuwafanya wahitimu kujenga ari ya kujifunza na wahitimu kuwa na ujuzi, mwelekeo chanya na kuwa na nia ya kujifunza zaidi.

"Tunatarajia kutoa mtoto wa ndoto yetu. Kila mmoja ana mhitimu wake wa ndoto yake kwamba akihitimu aje kuwa nani. Anapotoka amemaliza awe na maarifa kwa mwanafunzi aliyemaliza darasa la saba, kidato cha nne na sita.

"Rais alisema tuwajengee ujuzi wahitimu waweze kujiajiri, maoni haya yatasaidia kuwa na mitaala bora ili vijana wetu wajitambue, wawe na stadi za maisha," alisema.

Profesa Ndalichako alisema Tanzania inashirikiana na mataifa mengine kikanda na kimataifa hivyo ipo haja ya mitaala kuendana na mahitaji ikiwamo hali halisi ya mabadiliko ya kiteknolojia, kisayansi, kijamii na kwamba mitaala hiyo tangu uhuru imefanyiwa marekebisho mara tano.

"Bado kuna maoni kuhusu kuwapo elimu inayohitajika kwa manufaa zaidi, watu bado wana dukuduku la kwamba kuwe na mjadala wa kitaifa kuhusu elimu, mbali na mabadiliko ya mtaala mara tano.

"Wadau mtusaidie wizara kuwa na mtaala bora. Sasa huu ni wakati wa mjadala kuhusu elimu yetu," alisema.

Profesa Ndalichako alizitaka taasisi nyingine za elimu na vyuo kuwa mijadala kama hiyo nchini ili kuinua kiwango bora na kubadili mfumo wa elimu.

HABARI KITAIFA

# Kishindo cha wananchi Sabaya afikishwa kortini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMIA ya wananchi kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro walihudhuria mahakamani jana kushuhudia Lengai Ole Sabaya na washtakiwa wenzake watano, wakisomewa maelezo ya awali ya mashtaka mawili ya unyang'anyi wa kutumia silaha yanayowakabili.

Jana, Ole Sabaya, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, na washtakiwa wenzake, waliwasili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha majira ya saa 9:30 asubuhi wakiwa chini ya ulinzi mkali wa askari magereza.

Katika lango la geti la kuingia mahakamani huko, mamia ya wananchi walifurika kushuhudia tukio la kufikishwa mahakamani kwa washtakiwa hao.

Wananchi hao walikuwa wakiimba nyimbo mbalimbali na kupaza sauti zao kwa nguvu na wakati mwingine iliathiri shughuli za mahakama zilizokuwa zinaendelea kwa wakati huo.

Wakili Mkuu wa Serikali, Tumaini Kweka, alidai mahakamani kuwa upelelezi wa shauri hilo la jinai namba 66 la mwaka 2021 umekalimika na aliiomba kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali kwa washtakiwa hao mbele ya Hakimu wa Mhakama hiyo, Salome Msha, Wakili wa Serikali, Tarsila Gervas, alidai washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka mawili ya jinai.

Wakili Tarsila alidai kuwa Ole Sabaya na wenzake Februari 9 mwaka huu, walifika katika duka linalomilikiwa na Mohamed Saad, lililoko Mtaa wa Bondeni jijini Arusha na kuwaweka chini ya ulinzi watu wote waliowakuta dukani huko.

Alidai kuwa baada watu hao kuwekwa chini ya ulinzi, waliwalazimisha kulala chini kwenye sakafu huku wakiwapiga ngumi, mateke na makofi.

Wakili huyo alidai kuwa Ole Sabaya aliwashikia bunduku watu hao huku akiwatisha kuwa atawapiga risasi endapo watashindwa kumweleza wapi alipokuwa mmiliki wa duka hilo.

Alidai kuwa baada ya watu hao kukataa kumweleza Ole Sabaya alikokuwa mmiliki wa duka hilo, alimfunga kwa pingu mmoja wa watu waliokuwa kwenye duka hilo, Bakari Msangi, ambaye ni Diwani wa Kata ya Sombetini (CCM).

"Sabaya akiwa ameshika silaha mkononi, alimtesa Bakari Msangi, Diwani wa Sombetini, na alimtisha kumuua kwa kuwa alidai kuingilia shughuli zake alizokuwa akifanya sehemu hiyo na baadaye Ole Sabaya alimsachi na kumchukulia fedha kiasi cha Sh. 390,000, na simu aina ya Teckno.

"Pia alichukua fedha nyingine kiasi cha Sh. 35,000, mali ya Ramadhani Rashid," alidai.Awali, akiwasomea mashtaka yanayowakabili washtakiwa hao, wakili huyo alidai shtaka la kwanza la unyang'anyi kwa kutumia silaha linamkabili Ole Sabaya na wenzake Silvester na Daniel.

Inadaiwa Februari 9 mwaka huu, Mtaa wa Bondeni jijiji Arusha, washtakiwa waliiba fedha kiasi cha Sh. 390,000 mali ya Bakari Msangi na baada ya kufanya uhalifu huo, walimpiga mhusika makofi, ngumi, mateke na walitumia silaha kumtisha ili wabaki fedha walizoiba kwake.

Shtaka la pili kwa washtakiwa hao ni la unyang'anyi wa kutumia silaha, kinyume cha kifungu cha 87(A), Kanuni ya Adhabu Sura ya 16, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Ilidawa mahakamani huko kuwa Ole Sabaya, Silvester na Daniel, Februari 9 mwaka huu, katika Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, wote kwa pamoja waliiba simu moja aina ya Teckno na fedha kiasi cha Sh. 35,000 mali ya Ramadhani Rashid na baada ya kufanya uhalifu huo, walimpiga mhusika makofi, ngumi, mateke na walitumia silaha kumtisha ili wabakiwe fedha na mali walizoiba.

Wakili wa Upande wa Utetezi, Mosses Mahuna, aliiomba mahakama kuhakikisha upelelezi wa mashtaka dhidi ya washtakiwa hao unafanyika haraka na kupatiwa nakala ya mashtaka. Washtakiwa hao walikana mashtaka hayo na Hakimu Salome aliahirisha kesi hiyo hadi itakapotajwa tena Julai 2 mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Ole Sabaya na wenzake, walifikishwa mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Martha Mahumbuga, kusomewa mashtaka manne yanayowakabili likiwamo la uhujumu uchumi, rushwa, kuongoza genge la uhalifu na utakatishaji wa fedha.

Wakili Mkuu wa Serikali, Tumaini Kweka, aliiomba mahakama kuahirisha kusikiliza shauri hilo kwa kuwa upelelezi haujakamilika na Hakimu aliahirisha shauri hilo hadi Julai 2 mwaka huu.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni pamoja na msaidizi wake, Silvester Stanslaus, Enock Togolani, John Odemba, Daniel Gabriel na Waston.

Washtakiwa hao wanaendelea kukaa mahabusu katika Gereza la Kisongo.

## Nape ataka Puma ipendelewe kuagiza mafuta kutoka nje

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, ameihoji serikali kwa nini isitumie kampuni ya Puma ambayo ina hisa asilimia 50 kuagiza mafuta nje ili nchi ipate fedha na mapato.

Nape alihoji hilo jana bungeni jijini Dodoma wakati akichangia bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambayo inatarajia kupitishwa na Bunge Jumanne ijayo.

Alisema serikali ina hisa 50 ndani ya kampuni hiyo lakini inaagiza mafuta kupitia mfumo wa uagizaji wa pamoja kwa kutangaza zabuni na wanaoleta ni kampuni za nje.

"Hapa tuna kampuni yetu ya Puma asilimia 50 ni serikali hivi kwa nini tusiwatumie hawa hawa tukaagiza mafuta tukapata fedha na kodi ya mapato kwa sababu kampuni ipo hapa na serikali ipate, tumeachia kampuni za nje zilete na wakileta tukilipa wanaondoka zao," alisema.

Nape alisema Puma ikiagiza mafuta nje hakuna atakayeshangaa kwa sababu ni kampuni ya Tanzania na serikali ina hisa huko.

"Kampuni ya Puma ina uwezo wa kufanya manunuzi (ununuzi) kimataifa tuondoke na kuhangaika na hao. Twendeni tukaitumie kampuni yetu ya ndani tutapata fedha za ziada tutapata mapato na mambo yetu yatakwenda vizuri," alisema.

Kuhusu kampuni ya Tipper ambayo serikali pia ina hisa asilimia 50, mbunge huyo alisema wanaweza kuzitumia zikaleta vyanzo vingine vya mapato.

Alisema kwenye Tipper serikali ina miundombinu ya kuhifadhi mafuta na kupendekeza kuwa waruhusu wengine ndani ya serikali kutengeneza matangi mengine.

"Kuna hoja ya bandari kutaka kuingia huko hakuna sababu tutumie yale yale ya Tipper, kuna hoja ya TPDC (Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania) kwenda huko. Kila mmoja atimize wajibu wake. Kazi hii ya kupokea haya mafuta na kuyahifadhi waachiwe Tipper," alisema.

Alisema tangu kampuni ya Tipper imeanza, Mkurugenzi wake amekuwa akitokea Ufaransa lakini juzi kiongozi wake baada ya kujiuzulu na kutangazwa nafasi, waliomba watu watatu kutoka , mmoja kutoka India na Mtanzania.



# Waziri aipa mtihani Taasisi ya Uongozi

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, ameitaka Taasisi ya Uongozi kuweka uratibu na ratiba itakayowezesha viongozi wote wa umma walioteuliwa kupatiwa mafunzo.

Alitoa agizo hilo jana mkoani Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Taasisi hiyo, akisisitiza suala la kuandaa viongozi ni muhimu ili kuhakikisha wanajua majukumu yao na kuyatekeleza kwa weledi.

Waziri huyo alisema utendaji kazi unakwenda sambamba na maadili na kuzingatia kiapo walichopewa katika kutekeleza wajibu wao.

"Ndiyo maana leo (jana) wakati ninazindua hii bodi nimewakumbusha viongozi wetu wapya wa bodi maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Hassan Suluhu yanazingatiwa na yanatekelezwa," alisema.

Mchengerwa alisema maelekezo hayo yalishatolewa siku chache zilizopita, hivyo wanakipongeza chuo hicho kwa kuandaa miongozo na kuhakikisha wanatoa mafunzo kwa wakuu wote wa mikoa walioteuliwa pamoja na viongozi wengine wote.

Alisema wakurugenzi, makatibu wakuu wa wizara pamoja na mawaziri wanapaswa kupata mafunzo hayo muhimu kwa kila kiongozi wa umma aliyeteuliwa na kushika nafasi.

"Leo (jana) tulikuwa tunakumbushana, ni lazima chuo hiki kirejeshe sifa zake za kuwa chuo cha kutoa mafunzo kwa viongozi. Ukienda nchi nyingi za Afrika chuo hiki kina sifa nyingi sana," alisema.

Waziri huyo alisema viongozi wengi huandaliwa kupitia chuo hicho.

Alisema hakuna kiongozi wa umma ambaye ni wa mwisho katika utendaji wake wa kazi kwa kuwa kila kiongozi anatakiwa ajue anawajibika kwenye Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aliongeza kuwa hakuna kiongozi yeyote aliyeteuliwa au aliye kwenye madaraka yoyote, anapofanya majukumu yake ni vyema akazingatia mafunzo mbalimbali ambayo yatatolewa kupitia chuo hicho.

Aliongeza kuwa hategemei baada ya mafunzo haya kiongozi yeyote atende kinyume cha utendaji wa kazi unaokusudiwa na Rais Samia anayetilia mkazo utendaji wa kazi unaozingatia haki na maadili.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Stergomena Tax, alisema dhumuni kubwa la Taasisi ya Uongozi ni kujenga viongozi watakaoleta maendeleo endelevu kwa Tanzania.

Alisema siyo kwamba Tanzania haina viongozi, bali wanataka kuendana na mabadiliko ya dunia, hivyo lazima kuwe na viongozi watakaoleta maendeleo endelevu.

000



Katibu Tawala wa Wilaya Kigamboni, Dalmia Mikaya (wa pili kulia), akikabidhi zawadi kwa mwanafunzi wa Shule ya Msingi Ufukoni, Nasra Omary, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliofanyika wilayani Kigamboni, mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii. Kushoto ni Meneja wa Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA) Kanda ya Dar es Salaam, Victoria Huburys. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbowe, Lipumba wamuaga Baregu

**Na Jumanne Juma**

MWILI wa aliyekuwa mwanachama na mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Profesa Mwesiga Baregu, umeagwa mkoani Dar es Salaam na kusafirishwa kwenda Kagera kwa ajili ya maziko.

Jana, mwili wa mwanazuoni huyo mahiri uliagwa kwenye Kanisa la Kiinjili Kilutheri (KKKT) Kunduchi na baadaye kusafirisha kwenda mkoani Karega kwa maziko yanayotarajiwa kufanyika leo.

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, aliwaongoza waombolezaji kuaga mwili huo.

Mbali na Mbowe, viongozi wengine wengi wa kisiasa walihudhuria kanisani kuuaga mwili wa mwanazuoni huyo.

Viongozi wengine waliohudhuria ni pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF) Prof. Ibrahim Lipumba, John Cheyo wa UDP, Katibu wa Itikadi Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka na baadhi ya wabunge.

Msemaji wa familia alisema Prof. Baregu alianza kuugua kiharusi tangu mwaka 2019 kabla ya kukumbwa na umauti Mei 13, mwaka huu.

Mwili wa marehemu ulisafirisha kwenda Bukoba mkoani Kagera kwa ajili ya maziko. Profesa Baregu ameacha mke na watoto.

# RC apiga 'stop' kampuni kununua pamba

**Na Happy Severine,**
BARIADI.

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amepiga marufuku kampuni mbili zilizopewa vibali vya kununua pamba kuendelea kununua zao hilo katika msimu wa 2021/22.

Kafulila amezitaja kampuni hizo kuwa ni Chisano Co. Ltd ya Busega mkoani hapa na Birchard Co. Ltd kutoka jijini Mwanza.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari na kwamba sababu za kufikia uamuzi huo ni kutokana na kampuni hizo kudaiwa kuhusika katika kuhujumu mbegu za pamba ambazo zilitolewa na bodi ya pamba kwenda kwa wakulima.

Kafulila alisema kuwa kampuni hizo zilihujumu mbegu tani 20 ambazo zilikamatwa Novemba, mwaka jana katika Wilaya ya Busega zikiwa zinapelekwa kwa ajili ya kuchakata mafuta badala ya kwenda kwa wakulima.

Mbegu hizo zilikamatwa kwenye kiwanda cha Chisano huku zikiwa zimepakiwa kwenye gari la kampuni ya Birchard na zilikuwa zinapelekwa kwa wakulima lakini zikaenda kukamuliwa mafuta ya kula.

Aidha, Kafulila ameagiza vyama vyote vya msingi ambavyo vilikuwa vimepokea pesa kwa ajili ya kukusanya pamba kutoka kwenye kampuni hizo, visitishe mara moja na pesa hizo zirejeshwe.

"Kuanzia sasa ni marufuku kwa kampuni hizo kuendelea kununua pamba kwenye mkoa huu.

Najua walipewa vibali lakini ni kimakosa. AMCOS (vyama vya msingi vya ushirika) ambazo zilipewa pesa, kuanzia sasa zisitishe kununua na pesa zirejeshwe kwenye kampuni hizo," alisema

Kafulila alisema serikali haitawavumilia watu wote wanaohujumu wakulima au kukwamisha jitihada za serikali za kuboresha zao hilo.

Alisema hatua zingine kali za kisheria zitaendelea kuchukuliwa kwa watu wote ambao walihusika katika uhujumu wa mbegu hizo, ikiwemo wale ambao walisababisha mbegu hizo zichukuliwe badala ya kwenda kwa wakulima.

"Wako watu ambao walichepusha hizo mbegu nao hatua dhidi yao zitachukuliwa. Uchunguzi utafanyika kwa wahusika wote kuanzia bodi ya pamba," alisema Kafulila.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chisano, Peter Bahini, alikiri mbegu hizo kukamatiwa kwake lakini hakuhusika katika tuhuma hizo za uhujumu.

Uongozi wa Birchard ulipoulizwa, ulisema bado haujapata barua rasmi ya zuio hilo na kwamba ukiipata utazungumzia jambo hilo na kwamba kwa sasa hauwezi kusema chochote.

HABARI KITAIFA

# Rais Samia amtaka mwekezaji toka Malaysia kupanua uwekezaji kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alikutana na kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Kampuni ya Wilmar International ya Singapore, Kuok Khoon Hong.

Katika mazungumzo hayo, Hong ameahidi kuwa kampuni hiyo ipo tayari kupanua uwekezaji wake katika uzalishaji wa mchele na mafuta kwa kuwa mchele wa Tanzania ni bora na wenye soko kubwa duniani na mahitaji ya mafuta ni makubwa ndani ya nchi.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilisema Hong alisema kampuni hiyo imefurahishwa na dhamira ya Rais Samia ya kuwavutia zaidi wawekezaji.

Alikaririwa akisema tayari kampuni hiyo imeshawekeza nchini Dola za Marekani 150,000 katika kiwanda cha kusafisha mafuta ya kula, kutengeneza sabuni na tambi ikiwa ni sehemu ya uwekezaji wa takribani Dola za Marekani bilioni moja barani Afrika.

Kwa sasa, taarifa ilisema kampuni ya Wilmar imekamilisha kujenga kiwanda cha kukoboa mpunga na kufungasha mchele mkoani Morogoro kitakachokuwa na uwezo wa kukoboa tani 300 za mpunga kwa siku na kutoa ajira kwa zaidi ya watu 300.

Akizungumza na mwekezaji huyo, Rais Samia alimpongeza Hong kwa uwekezaji wake nchini na amemkaribisha kupanua zaidi uwekezaji huo hususan katika uzalishaji na usindikaji wa mafuta ya alizeti, michikichi na kilimo cha umwagiliaji.

Rais Samia alimweleza kuwa Tanzania iko tayari kushirikiana na kampuni hiyo katika uwekezaji huo na ameagiza Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha na Mipango kuandaa andiko la pamoja na kampuni hiyo litakalowezesha ushirikiano huo hususan katika kupata teknolojia, mbegu na mitaji.bAidha, Rais Samia alitoa wito kwa wawekezaji wengine kuwekeza nchini hasa katika sekta ya kilimo kwa kuwa Tanzania ina eneo kubwa linalofaa kwa kilimo lakini halitumiki ipasavyo.

Mazungumzo hayo yalihudhuriwa na Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, Balozi wa Tanzania nchini Malaysia, Dk. Ramadhan Dau, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango,Emmanuel Tutuba na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata.

# Makinda amrithi Dk. Salim Kairuki

**Na Christina Mwakangale**

SPIKA mstaafu, Anne Makinda, ameteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) akichukua nafasi ya Dk. Salim Ahmed Salim.

Hafla ya kumsimika rasmi kwenye nafasi hiyo, ilifanyika jana chuoni hapo, Mikocheni, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa chuo hicho.

Akizungumza baada ya kusimikwa, Makinda alisisitiza maadili na nidhamu kwenye vyuo vikuu hususan vinavyotoa elimu ya tiba na uuguzi kwa kuwa vitasaidia wahitimu wa kada ya afya kutoa huduma zilizo bora na haki.

Pia alisema vyuo hivyo hususani vya binafsi, vibadili changamoto za kiuchumi vilizo nazo na kuwa fursa ili kuongeza ufanisi na ushindani kwenye soko.

Alisema mafunzo pamoja na vyeti pekee haitoshi kumtambulisha mhitimu wa chuo kikuu kuwa bora, bila kufuatwa kanuni za maadili katika utendaji kazi zao za kuhudumia jamii.

"Nidhamu pekee inaweza kukifanya chuo kuwa chenye ubora, mafanikio pia yanatokana na nidhamu, huwezi kuwatendea visivyo wenzio ukiwa kwenye majukumu yako ukiwa nidhamu. Nidhamu inaogopa," alisema Makinda.

"Nilikutana na baadhi ya wanafunzi wa chuo hiki, nikaona kabisa na nidhamu, hiyo ni muhimu sana, nidhamu maadili kwa wanafunzi ni kitu cha kwanza. Nilipokuwa India siku za nyuma, baadhi ya wadau waliniambia watafungua chuo cha wauguzi, kwa sababu wanasikia baadhi yao hawana nidhamu," alisisitiza.

Pia alisema pamoja na wahitimu wa sekta ya afya baadhi yao kutokuwa na ajira, bado watoa huduma hawa wanahitajika kwenye jamii na taifa kwa ujumla.

Kadhalika, Makinda alitoa wito kwa chuo hicho kubuni vyanzo vya mapato, badala ya kutegemea chanzo pekee cha ada kutoka kwa wanafunzi, huku akishukuru chuo hicho kwa kumchagua kuwa mkuu wa chuo.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa chuo hicho, Kokushubila Kairuki, alisema kuwa anaiomba serikali iangalie namna ya kuvisaidia vyuo binafsi kwa kuwapatia fedha ili kuinua ufanisi wa vyuo nchini.

"Nina imani wahitimu wa vyuo binafsi, kikiwamo Kairuki wakitoka hapa wanakwenda kuhudumia jamii hivyo tunaiomba serikali isaidie kutoa fedha kwa vyuo binafsi. Pendekezo hili linaanzia kwa mkuu wetu mpya, Makinda, tunafahamu uzoefu ulionao katika uongozi na una ushawishi," alisema Kairuki.



Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki (HKMU), John Ulanga, akimvalisha kofia Mkuu mpya wa Chuo hicho, Anne Makinda, kama ishara ya kumsimika rasmi kwenye nafasi hiyo, mkoani Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Afya na Elimu la Kairuki, Kokushubila Kairuki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aibua staili mpya kudai kodi

**Na Rose Jacob, MWANZA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, ameibuka na staili mpya ya kudai madeni ya kodi ya majengo baada ya kuingia katika ofisi za umma na binafsi akiongozana na maofisa wa serikali.

Hatua hiyo ya Dk, Angelina inatokana na wadaiwa hao kushindwa kulipa madeni yao ya kodi ya majengo katika Mkoa wa Mwanza.

Hivi karibuni, mahakama ilitoa amri kwa ofisi ya Kamishina wa Ardhi mkoani Mwanza kutaifisha viwanja vya watu walioshindwa kulipa kodi na kuviuza kwa mnada.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Dk. Mabula alisema wameamua kutumia busara ya kufika kwa wamiliki wa ardhi ambao ni wadaiwa sugu ili kujua matatizo gani yaliyosababisha washindwe kulipa kodi kwa wakati.

"Nimeamua kutembelea maeneo ambayo wamiliki wake wanadaiwa madeni makubwa, nimebaini wengi wanahusisha jamii kubwa, mfano shuleni na kwenye taasisi binafsi na serikali, hivyo tukipiga mnada tunakuwa tumeathiri familia nyingi ndiyo maana hatutaki kutengeneza migogoro baina ya serikali na wananchi.

Tumezungumza nao, baadhi wamelipa wengine wameomba kulipa kwa awamu," alisema.

Naibu Waziri aliagiza watendaji wa sekta ya ardhi kuhakikisha wanawahamasisha wananchi wanaodaiwa kodi, kulipa kidogo kidogo kuliko kuwaacha wanajisahau hadi wanajikuta fedha zimekuwa nyingi.

"Wananchi wapewe elimu juu ya ulipaji kodi na kujua sheria zinavyoelekeza ili mtu awe makini katika kukabiliana na deni analodaiwa, maana sheria namba 33 kifungu kidogo cha kwanza, inampatia idhini kamishina hususan ka ndani ya miezi 6 atamfutia," alisema

Kaimu Kamishina wa Ardhi mkoani Mwanza, Elia Kamihanda, alisema wamefanya ziara na kuwafikia wadaiwa sugu 20, ambao deni wanalodaiwa ni la miaka miwili kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 1.4 katika wilaya za Ilemela na Nyamagana.

"Ziara hii imezaa matunda kutokana na wadaiwa hao wengine kulipa maduhuri na wengine wameomba kulipa kwa awamu tatu kuanzia Julai, mwaka huu, tunawashauri wafanye hivyo bila kushurutishwa maana si vizuri tukitumia nguvu ambayo itawaathiri wao, sisi hatutaki mambo hayo tunataka kujenga uhusiano mzuri ambao unaleta maendeleo kwa serikali na wananchi wake," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa hili Metacha anatakiwa aombe radhi

**MARA** baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga dhidi ya Ruvu Shooting kumalizika, baadhi ya mashabiki walionekana kumzomea kipa, Metacha Mnata.

Mashabiki wa Yanga walionekana kukasirishwa na kile walichokiona kuwa kipa wao huyo alifungwa mabao mawili ya kizembe. Kwenye mechi hiyo ambayo Yanga ilishinda mabao 3-2.

Mechi ilipomalizika ilionekana kana kwamba Yanga ndiyo imefungwa. Mashabiki walionekana kucharuka, wakimzomea kipa huyo, wengine walimtolea maneno makali.

Inaonekana kabisa kuwa kipa huyo alishindwa kuwa mvumilivu. Alirudishia kwa kuwaonyesha ishara ya kidole cha kati ambacho kwenye jamii huwa kina tafsiri ambayo si nzuri.

Kitendo kile badala ya kupoza moto, ilikuwa kana kwamba ndiyo amemimina petroli kwenye moto unaowaka.

Ni kweli kwenye akili yake Metacha anaona ni kama mtu anayeonewa kwani amefungwa mabao hayo kimpira tu, lakini kwa mashabiki siku zote huwa na tafsiri zao kichwani na wala si watu wa kubishana nao.

Mchezaji hawezi kubishana au kushindana na kundi la watu ambao siku zote wanachojua wao ni kitu kimoja tu, ushindi na wanapoona kuna dalili za mtu au mchezaji ambaye anaweka ugumu kwenye ushindi wao, basi kila mmoja atasema na kufanya anachokitaka.

Si Tanzania tu. Hata Ulaya, mashabiki wa klabu ndiyo huwa na nguvu zaidi kuliko hata klabu yenyewe wala wachezaji.

Hawa ndiyo wanaofanya klabu iwe pale ilipo. Wananunua bidhaa, ikiwemo jezi, skafu na vitu vingi, ikiwemo hata kulipa fedha za kuingia viwanjani na kuishabikia klabu kupata fedha nyingi.

Hakuna kiongozi wa klabu yoyote atakayemtetea mchezaji mbele ya mashabiki. Kwa sababu viongozi na wachezaji hupita, lakini shabiki atabaki na timu hiyo milele.

Ndiyo maana mara baada ya tukio la juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, uongozi wa Yanga ulitoa tamko la kumsimamisha kipa huyo kwa muda usiojulikana, lakini pia kuomba radhi kwa wanachama na mashabiki kuhusu tukio lililotokea.

Kina Cristiano Ronaldo, Lionel Messi ambao ni wachezaji bora kabisa duniani, siyo kwamba wamefika pale kilelemama, wamepitia maswahibu mengi ikiwemo kuzomewa, si na timu pinzani tu, wakati mwingine mpaka na klabu zao wenyewe.


Mfano Messi amekuwa akikumbana na hali kama hiyo anapokwenda kucheza kwenye timu ya taifa ya Argentina na kutofanya vema, zomeazomea na lawama zote zimekuwa zikimwangukia yeye, lakini hakuna hata siku moja ameonekana anarudishia.

Kuna baadhi ya wachezaji Ulaya wamewahi kukumbwa hata na kadhia ya kuvamiwa nyumbani kwao na makundi na mashabiki wakiwa na mabango kupeleka ujumbe, lakini kwa sababu wamekomaa na kufundishwa misingi ya soka, huwa hawajibu, badala yake tu kupiga ripoti polisi ili kuwaondoa.

Nipashe tunaamini kwa hili, Metacha naye ataangalia uwezekano na kuandika waraka wa kuomba radhi kwa sababu si kitendo cha uanamichezo.

Tunamini kuwa Metacha atakachofanya baada ya kuomba radhi na kukaa na kuangalia upungufu wake na kuufanyia kazi, si kwa manufaa ya klabu ya Yanga tu, hata yake mwenyewe kwenye karia yake ya soka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wagombea wengi urais TFF hawakujipanga

Na Adam Fungamwango

**NI** wazi kuwa baadhi ya wagombea urais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) hawakujipanga kisawasawa kwa ajili ya kinyang'anyiro hicho.

Mpaka sasa Kamati ya Uchaguzi wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) chini ya Mwenyekiti wake, Wakili Kiomoni Kimamba, imewaengua baadhi ya wagombea wa uraia wa Shirikisho hilo, kuelekea kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Agosti 7, jijini Tanga.

Ni wagombea watatu tu ambao wamepitishwa, akiwamo anayetetea kiti chake kwa mara nyingine tena, Wallace Karia.

Waliopitishwa kupambana na mtetezi wa kiti hicho ni Hawa Mninga na Evance Mgeusa.

Baadhi ya walioenguliwa ni Oscar Oscar na Ally Mayay ambao walionekana kama wangeweza kuleta ushindani kwenye kinyang'anyiro hicho.

Awali, ilionekana kama Mbunge wa Jimbo la Kinondoni Abbas Tarimba ambaye alichukuliwa fomu na Mayay angeweza kuwa mshindani wa ukweli wa rais wa sasa, Karia, lakini hakurudisha fomu.

Wengi wa wagombea, mbali na vigezo vingine, lakini tatizo kuwa lilikuwa na kupata wadhamini.

Hili ndilo limekuwa tatizo kubwa sana lililoonekana kwa wagombea wengi kwenye uchaguzi huo.

Hata hivyo, ukiangalia ni kwamba suala la kupata wadhamini kwenye uchaguzi wa Shirikisho hilo limekuwa ni la muda mrefu. Kuna vitu vichache tu ndivyo vimekuwa vikirekebishwa hapa na pale, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa udhamini umekuwa ukitolewa kwa wagombea kwenye chaguzi zote.

Lakini kutokana kuwa ngumu kuwapata kwa wagombea wengi kwenye uchaguzi huu, imeonekana kama ndiyo limeanza kuwa tatizo kubwa limewakwamisha wagombea wengi.

Ni kweli limewakwamisha, lakini baadhi ya wagombea kwenye uchaguzi huu huu wamepata udhamini.

Na si huu tu, hata chaguzi zilizopita baadhi ya wagombea wamekuwa wakinyang'anyana wadhamini na viongozi waliopo madarakani.

Kwa jinsi ninavyoona mimi ni kwamba, wagombea wengi safari hii hasa wale walioonekana kwa mashabiki wengi wa soka wanakwenda kumpa upinzani mkubwa Rais Karia hawakuwa wamejipanga.

Ni kama vile wameshtukizwa wakati uchaguzi umekaribia na si tangu awali walijipanga kwenye uchaguzi. Au kuna watu walifuata na kuwataka wakachukue fomu wagombee kwa ajili ya kutaka kumuondoa Karia madarakani tu.

Hakuna kiongozi aliye madarakani anayeweza kushindwa kizembe hivyo.

Ikumbukwe kiongozi yoyote aliye madarakani, huanza uchaguzi mwingine mara baada ya kuingia madarakani, hivyo yoyote anayetaka kushindana naye ni lazima aanze kujipanga na yeye kipindi hicho.

Wakati akiweka viongozi mikoani, watu huanza kuwazungukia na kuwaweka sawa kwa siri wakati yeye yupo madarakani na ukifika wakati wa uchaguzi, yeye mwenyewe kiongozi aliyekuwa madarakani anashtukia tu amegeukwa na muda haupo tena.

Karia angeweza kupata wakati mgumu kama angepata mpinzani ambaye alikuwa amejipanga kwa muda mrefu kuwa kiongozi wa TFF.

Kuna watu wanasema kuwa kwa jinsi kanuni zilivyoyowekwa ni ngumu mno kupita kwenye mchujo na kushinda.

Achilia mbali hawa ambao wao wamepata wadhamini na kupita, huko nyuma kwa kanuni hizi hizi kulikuwa na wagombea ambao kama wangekuwa hivi sasa wangeweza kabisa kumshinda na Karia na hata kung'oa.

Kwenye uchaguzi kama huu, hawakuwepo watu kama Michael Wambura, Ismail Aden Rage, Jamal Malinzi, na wengineo wenye kaliba kama hiyo ya 'roho ya paka,' ambao wakilitaka jambo lao, hata kanuni iwe ngumu vipi wao watapenya tu.

Ni watu ambao hujipanga muda mrefu wanapotaka uongozi, lakini pia wanakuwa na ushawishi na kuaminika, hivyo kwa kanuni ambayo imeonekana kuwa ngumu kwa wengine kwa wao ingekuwa rahisi zaidi.

Nadhani imefika wakati sasa baada ya uchaguzi kumalizika, yoyote anayetaka kuiongoza TFF aanzie hapo. Aanze kujiandaa na uchaguzi ujao, ikiwamo kuhoji na kushinikiza baadhi ya kanuni zibadilishwe au kurekebishwa. Wadau wa soka waungane kurekebisha upungufu uliokuwepo na si kusubiri hadi uchaguzi ukaribie.

Vinginevyo wagombea walioshindwa, wakiendelea kukaa kimya baada ya uchaguzi, tutaona kabisa kuwa lengo halikuwa kuiongoza TFF, bali ilikuwa ni kumuondoa tu Karia.

BURIANI MWESIGA BAREGU

# Maisha yote hakuwahi kuweka kando uprofesa, taaluma yake

## ■Haya hapa usiyoyajua kuhusu mwanazuoni huyo

**Na Peter Orwa**

NI wiki inayobeba simanzi kwa kada ya wanataaluma, siasa na nje ya hapo, kuanzia mzizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ambako mwanazuoni wake mkongwe Prof. Mwesiga Baregu, leo anawekwa kwenye nyumba ya milele mkoani Kagera, baada ya kuagwa jana nyumbani kwake, Dar es Salaam.

Ni ngumu kumtafsiri Prof. Baregu katika eneo au matendo mawili au matatu, kwa kuwa ana mengi. Wasifu wa kipekee, ni msomi 'kindakindaki' wa Sayansi ya Siasa, mahsusi uhusiano wa kimataifa, akijikita katika uhusiano uchumi.

Taasisi za elimu ya juu zikiwajibika kushauri, kutafiti, pia kufundishaji, mtekelezaji huyo alizama vilivyo.

Nafsi yake alijulikana mwenye msimamo na 'kutobabaishwa' kwa alichoamini na ilijulikana kwa wengi. Lakini, kwenye mjumuiko kitaaluma kama darasani, alikuwa mwingine; rafiki mchekeshaji na vituko kibao.

Kihistoria, maisha yake alipenda kubaki ndani ya kijiji cha wasomi , historia kuu ikiwa chuo kikuu Mlimani, ikiwamo kijiwe cha jioni, Klabu ya UDASA.

**MAISHA YA DARASANI**

Prof. Baregu, mfumo wake darasani alianzisha kwa 'michapo' ndani yake ina mantiki kitaaluma au ndani ya anachofundisha, ndipo anaendelea na anachonuia.

Hapo inaendana na weledi wa Kiingereza, kiwango cha kushangaza wasomi wenzake. Mvuto mkuu ni anapokutwa na kigugumizi kukumbuka jambo, hapo 'bomba' linalofuata sharti msikiaji akatafute kamusi.

Katika hilo, huko nyuma aliwachekesha wanaomjua alipokaririwa gazetini akijieleza alifeli Kiingereza shuleni.

Ninakumbuka mmoja wa maprofesa wa UDSM aliyekuwa naye idara moja alinitamkia "Hicho mnachosema (magazeti) hakiwezekani, yumo hata katika 10 bora ya Kiingereza Mlimani."

Leo hii yanapotajwa majina makubwa ya kitaaluma kama Mkuu wa Taaluma UDSM, Prof. Bernadeta Kilian na Balozi Dk. Benson Bana ni wanufaika wa mchango wa Prof. Baregu.

Pia, aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Siasa na Utawala wa Umma UDSM, Dk. Bana, aliwahi kutamka Prof. Baregu alikuwa tegemeo lao katika kuanzishwa shahada ya uzamivu (PhD). Bahati mbaya aliondoka baada ya kushiriki kuandaa.

Kuna historia inayokaribia miongo mitatu imeacha kumbukumbu kwa tukio mwanafunzi aliyecharuka kumropokea darasani kulaumu utungaji wake majaribio, jambo lililowatia hofu wenzake huenda profesa angemchukulia hatua kali.

Iliwashangaza, kinyume cha yule Baregu wanaomfahamu, alitoa majibu laini anavyopaswa kujiandaa.

Hata aliporudia mara ya pili, alimkosoa kwa ukali kidogo, ila akamrejeshea ujumbe wa upendo akimfananisha na binti zake. Hilo liliacha gumzo.



Marehemu Profesa Mwesiga Baregu. **PICHA: MTANDAO.**

**MIJADALA TAALUMA**

Alihusudu mno mijadala ya taaluma maarufu 'panel discussion' iliyozama katika mada yanayojiri kitaifa wakati huo na kwa kiasi kikubwa wadau wake kutoka Kitivo cha Sanaa Jamii, wenyeji zaidi ni Idara ya Sayansi ya Siasa anakotoka Prof. Baregu, Taasisi ya Taaluma ya Maendeleo (IDS) na Kitivo cha Sheria.

Bado ninakumbuka sana mjadala wa kitaaluma mwazoni mwa miaka 1990 uliojadili kuwapo serikali tatu nchini, ikiwamo Tanganyika, ukipewa jina 'Whither Tanganyika'.

Hapo ndipo nilipobaini umahiri wake Baregu, nikioanisha na anavyosifiwa ndani na nje ya Mlimani. Ilikuwa kipindi wabunge 55 maarufu 'G 55' walioshinikiza kuwapo Serikali ya Tanganyika, zama za Bunge la chama kimoja.

Mjadala uliundwa na wajumbe watano, mwenyekiti alikuwa mkongwe wao kiumri na kitaaluma, Prof. Samwel Mushi, wawasilishaji; Jenerali Ulimwengu, mwanasheria mhitimu wa UDSM, mwanahabari, mwanasiasa na mweledi wa mambo ya jamii, alipokuwa mbunge.

Jenerali alitakiwa kuainisha kinachojiri bungeni, lakini hakuhudhuria na aliwasilisha kimaandishi baada ya kupatwa na udhuru wa familia.

Wengine wote kutoka UDSM, walikuwa Prof. Haroub Othman, mbobevu kutoka IDS, aliyedadavua siasa ya nchi kwa mifano na msukosuko kabla na baada ya uhuru, akiwashangaza wasikilizaji wasomi, marejeo yake ni karatasi isiyojaa kiganjani, lakini hoja iliyopitiliza.

Akafuatiwa na Prof. Baregu, aliyechambua siasa nchini, kisha Dk. Ringo Tenga akiainisha taswira ya siasa kisheria.

Prof. Baregu mbali na kuchekesha, alikuwa na matatu aliyoyatambulisha kwa kutumia 'kizungu kilichoenda shule' zikibeba dhana kuu, 'will' akimaanisha uwezekano, 'necessity' umuhimu na mwisho 'prevalence' kwamba ni kuenea au kushamiri.

Aliziweka kuwa mwongozo wa kujenga hoja zake.

Kauli yake ya Kiingereza kwa tafsiri yake sisi ni kwamba: "Ili siasa iweze kuishamiri kunatakiwa kuwapo 'uwezekano' pia 'umuhimu'.

"Siku zote 'uwezekano' unadumu kuushikilia 'umuhimu', pia 'umuhimu' nao una nafasi pale kustawisha 'uwezekano.' Kuwapo ubia kati ya'uwezekano'na 'umuhimu' ndiyo unawezesha siasa kushamiri..."

Ni hoja iliyowaachia butwaa kundi la wasomi wengine waliodumu kungoja zamu zao kuongea, ikibeba orodha ya maprofesa wabobevu kama, mwanahistoria Wamba dia Wamba na mwanasosholojia, Sethy Chachage.

'Nondo' za Prof. Baregu ziliendeleza butwaa pale alipolichukulia hilo la 'will' na 'necessity' kama rasharasha akiwatamkia wajumbe: "sasa ndiyo ninaanza..." hatua aliyotumia kujadili hoja hizo tatu kujumuisha anachokijadili kisiasa.

Hapo alirejea mtazamo wake katika mjadala wa 'G55'na Serikali ya Tanganyika akioanisha na nafasi ya ama 'will' au 'neccesity' huku akirushia 'vijembe' vya kitaaluma kuwakosoa wanasheria.

Mara nyingi masihara yake alimfikishia Dk. Ringo Tenga, akitamkia kwa kumshika bega: "sioni 'will' hapa, labda mwanasheria jirani yangu anajua zaidi..."

Ilipokuja zamu ya Dk. Tenga, naye alijitetea kitaaluma akimkosoa Baregu, pale alipofafanua majumuisho yake kwa mtindo wa hukumu mahakamani kwa kurejea njia za Baregu, safari hii naye alimtia 'hatiani' akimshika na kumhoji: "je hii ni necessity?'

Prof. Baregu 'alipotiwa hatiani' mara kadhaa na Dk. Tenga, alishika kichwa kuashiria kujutia kumchokoza mwanasheria Dk. Tenga, hata mwisho akakiuka kanuni na utamaduni wa 'panel discussion' kuwa ya Kiingereza pekee, Prof, Baregu akaropoka Kiswahili akishikilia kichwa "...huyu mwanasheria anataka kunimaliza jamani!"

Hapo akazua kicheko kwa wahudhuriaji, wa kikao hicho kilichodumu hadi saa sita usiku.

Inasikitisha katika waliotajwa, walio hai leo ni Dk. Tenga na Jenerali.

**HAKUIHAMA TAALUMA**

Daima Prof. Baregu aliipenda kazi ya taaluma na hakuwahi kuihama, kwa upekee fani yake sayansi ya siasa.

Alijivunia kitaaluma kuumbwa na Profesa Abdulharman Babu, naye akamtengeneza mrithi katika eneo lake la ubobevu Profesa Mohabe Nyirabu.

Katika miaka ya 1990, ana historia ya kutakiwa kuteuliwa balozi, inasemekana alikataa.

Ila baadaye, 'uzalendo ulimshinda' mwanzoni mwa miaka 1990, alijiunga rasmi katika siasa, chama cha NCCR Mageuzi na baadaye CHADEMA akapewa nafasi za juu, lakini bado akawa mtaalamu mshauri aliyewasaidia, bila kuhama darasani.

Kifalsafa, ni muumini wa siasa mrengo wa kushoto, akiwahusudu sana wanafalsafa kama Che Guavara, hata mavazi yake alikuwa adimu kuchomekea shati, akimtambulisha ndivyo walivyokuwa na rafiki mbia wake, mwanasheria Prof. Haroub Othman.

Baregu alibaki rafiki wa wanafunzi vyuo vikuu na kuna wakati alihamia penye mlo wao mchana UDSM, kulipokuwapo mama lishe maarufu Mama Chiluba.

Ana mengi ya kukumbukwa, daima hakuacha uanataaluma maishani mwake. Mara ya mwisho alitumikia Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Dar es Salaam.

**Mungu alilaze mahali pema roho yake. Amina.**

# Raia wa China huru kesi uhujumu uchumi

Na Kulwa Nzee

RAIA sita wa China waliokuwa wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi kwa kukutwa na ndege aina ya tausi wameachiwa huru baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuomba mahakama ifanye hivyo. Washtakiwa hao waliachiwa jana na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu.

Akiiwakilisha Jamhuri, Wakili wa Serikali, Kiza Luzugana, alidai kesi ilikuja kwa ajili ya kutajwa lakini DPP aliwasilisha hati ya kuonyesha kwamba hana nia ya kuendelea na shauri hilo.

Washtakiwa walioachiwa huru ni Jin Erhao (35) anayejishughulisha na usafirishaji, Chengfa Yang (49) mfanyabiashara, Ren Yuangqing (55) Mkurugenzi wa Kampuni ya Usafirishaji ya Sinota, Shu Nan (50) mfanyakazi katika kampuni hiyo, Chen Shinguang (45) Meneja katika kampuni hiyo na Gu Jugen (57) Meneja Ufundi. Washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na mashtaka matatu likiwemo la kukutwa na tausi.

Baada ya kuwasilisha maombi hayo, Hakimu Chaungu alikubali na kuwaachia huru washtakiwa.

Kwa mujibu wa mashtaka, washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na kesi ya uhujumu yenye mashtaka matatu.

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa kwa moja wanadaiwa Agosti 11, 2020, Mtaa wa Sokoine kwa pamoja na kwa makusudi walisimamia genge la uhalifu lililosababisha kupatikana kwa ndege mmoja aina ya tausi mwenye thamani ya Sh 1,150,000.

Katika shtaka la pili, siku na eneo hilo, washtakiwa kwa pamoja walikutwa na nyara ya Serikali, iliyopatikana kinyume cha sheria ambayo ni ndege Tausi.

Shtaka la tatu, siku na maeneo hayo, kwa pamoja washtakiwa walikutwa na tausi huyo huku wakijua kuwa kumiliki ndege huyo ni kinyume cha sheria.

# Waziri aiomba UNDP kusaidia sekta ya ardhi

Na Munir Shemweta

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameliomba Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kusaidia juhudi za wizara katika kuendeleza sekta ya ardhi nchini.

Lukuvi aliwasilisha ombi hilo juzi wakati wa mazungumzo yake na Mwakilishi Mkazi wa UNDP nchini Tanzania, Christine Musisi, yaliyofanyika ofisi za wizara katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba jijini Dodoma.

"Ili kuiwezesha wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ni vyema tukawa na ushirikiano thabiti na UNDP kusaidia juhudi za wizara zenye lengo la kuleta matokeo chanya kwenye maendeleo ya ardhi," alisema Lukuvi.

Waziri Lukuvi alisema ushirikiano kati ya wizara na UNDP utaisadia Tanzania kufikia malengo namba 11 yatakayoifanya miji yake kuwa salama kufikia mwaka 2030.

Kwa mujibu wa Lukuvi, hivi sasa wizara inatekeleza mpango wake wa miaka 10 wenye lengo la kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi, hivyo kuboresha usalama wa miliki za ardhi kwa Watanzania.

Aidha, aliliomba shirika hilo kuangalia uwezekano wa kuisadia wizara yake vifaa vya upimaji na magari kwa lengo la kurahisisha kazi za upimaji kwenye maeneo mbalimbali jambo alilolieleza kuwa litaisadia pia kutatua migogoro ya ardhi.

Waziri pia alimweleza Musisi kuwa utekelezeji mpango kabambe nchini Tanzania bado una changamoto kwenye mamlaka za upangaji suala alilolieleza linasababisha maandalizi ya mipango kwenye mamlaka za serikali za mitaa kutoenda kwa kasi kutokana na ukosefu wa fedha na wataalamu wa kutosha. " Kwa sasa wizara imeidhinisha jumla ya mipango kabambe 26 katika miji sita, manispaa 13 pamoja na halmashauri za miji saba" alisema Lukuvi.

Kuhusu Kongamano la Kitaifa la Miji, alisema kongamano hilo ni muhimu kwa kuwa linajumuisha mijadala inayohusu masuala ya sera juu ya maendeleo endelevu ya miji katika ngazi ya kitaifa hasa kwenye utekelezaji agenda mpya ya miji na malengo ya maendeleo endelevu.

Naye Musisi alisema shirika lake litaangalia namna ya kuisaidia wizara katika masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi nchini ili kuifanya sekta hiyo kupiga hatua.

Musisi aliyeambatana na ujumbe wake katika ziara yake alisema, timu yake itakaa na timu ya wizara kuangalia maeneo yote ambayo shirika lake linaweza kusaidia ikiwamo kongamano la kitaifa kuhusiana na masuala ya miji.



Baadhi ya wanawake wakifuatilia kwa makini, wakati Benki ya NMB ikizindua klabu ya Jasiri (NMB Jasiri Club) mjini Mtwara, yenye nia ya kuendeleza upatikanaji wa mazingira mazuri ya kibiashara kwa wanawake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara yakanusha kuingizwa mayai toka nje

Na Elizabeth Zaya

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imesema hakuna mayai kutoka nje ya nchi ambayo yameingizwa nchini kama ambavyo imedaiwa na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, hakuna uingizaji wa mayai kutoka nje ya nchi uliosababisha kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo katika ngazi ya mfugaji na sokoni.

"Juni 14, mwaka huu, Wizara iliona ujumbe ukizunguka kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kuingia kwa mayai mengi nchini kutoka nje kiasi cha kusababisha kushuka kwa bei ya mayai mpaka kufikia Sh.4,000 kwa trei. Ujumbe huu ulikuwa ukisomeka 'soko la mayai DSM kitendawili.

"Baada ya kuona ujumbe huo, Juni 16, mwaka huu, wizara ilifanya uchunguzi kwenye makao makuu ya mikoa 26 nchini na baadhi ya wilaya ili kujiridhisha juu ya upatikanaji wa mayai.

Baada ya uchunguzi huo, ilibainika kwamba kinachoonekana ni upungufu wa mayai nchini ambao umesababisha bei ya bidhaa hiyo kupanda hadi kufikia Sh.12, 000 kwa trei na si Sh. 4,000 kama ilivyoakuwa ikisambazwa kwenye mitandao.

"Taarifa zilizosambazwa ni uzushi na hazina ukweli wowote kwa sababu serikali ilishazuia uingizwaji wa kuku na mazao yake kutokana na tishio la uwapo wa ugonjwa wa mafua na ndege duniani. Wizara imekuwa ikitoa vibali maalum vya kuingiza vifaranga na mayai ya kutotolesha ya kuku wazazi. Kwa hiyo taarifa hizo za uzushi zipuuzwe," ilisema taarifa hiyo.

Ndaki alisema suala la uhaba wa vifaranga nchini linafanyiwa kazi na kwamba kufikia Septemba mwaka huu litakuwa limetatuliwa na kurudi katika hali ya kawaida.

Kuhusu ugonjwa wa homa ya nguruwe nchini, Ndaki alisema wizara imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuudhibiti na kwamba mpaka kufikia mwishoni mwa Aprili, mwaka huu, katika mikoa mingi nchini hakukuwa na matukio ya ugonjwa huo.

"Januari 23, mwaka huu, nilitoa taarifa kwa umma juu ya uwapo wa mlipuko wa ugonjwa wa homa ya Nguruwe katika maeneo ya mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga na Dodoma na niliwaagiza wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri, kusimamia utekelezaji wa masharti ya karantini zilizokuwa zimewekwa na wataalamu wa mifugo, nawashukuru sana kwa jinsi walivyosimamia kazi hiyo," alisema Ndaki.

"Juni Mosi, mwaka huu, katika Manispaa ya Morogoro kulijitokeza matukio ya nguruwe 14 kufa na uchunguzi wa kimaabara ulionyesha ni ugonjwa wa homa ya nguruwe.

"Tayari juhudi kubwa za kuudhibiti zinaendelea ambazo ni pamoja na kuweka karatini ya kuingiza na kutoa nguruwe na mazao yake katika Manispaa hiyo na elimu inatolewa kwa wafugaji na wadau wengine kuhusu njia za kukinga ugonjwa usiingie kwenye mabanda ya mifugo hiyo. Mpaka kufikia juzi, hali ya ugonjwa katika Manispaa ya Morogoro imedhibitiwa na hakuna kifo tena kilichotokea kwa Nguruwe," alibainisha Ndaki.





Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar, Asiya Mwadini akichangia bajeti kuu ya Serikali, Bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vilio kuondoa VAT kwenye pedi vyaanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BAADA ya serikali kuondoa na kurudisha tena kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye taulo za kike, wadau wameishauri kuondoa tena VAT ili bidhaa hizo zipatikane kwa bei nafuu.

Mkurugenzi wa asasi ya kirai inayojishughulisha na masuala ya hedhi na afya ya uzazi salama ya ANUFLO, Flora Njelekela, alitoa ushauri huo jana akizungumza na waandishi wa habari kuhusu matembezi ya hisani ya kuhamasisha hedhi salama yatakayofanyika leo jijini hapa.

Alisema lengo ni kusaidia watoto wa kike waliopo shuleni wanaoshindwa kujistiri wakiwa kwenye siku zao za mwezi.

Mkurugenzi huyo alihamasisha wabunge na serikali kulipa kipaumbele suala la hedhi salama kwa kuwa mwaka 2018 waliondoa VAT lakini baadae ilirudishwa.

Alisema matembezi hayo yanalenga kukaa na wabunge kwa ajili ya kuwaomba waone ukubwa wa suala la hedhi salama na kero ambazo watoto wakiwa shuleni wanapitia.

"Tumeandaa matembezi haya ambayo mgeni rasmi ni Naibu Spika, Dk.Tulia Ackson na yataanzia viwanja vya bunge hadi Nyerere Square, wadau tuungane katika kumuinua mtoto wa kike,"alisema.

Njelekela alisema kwenye shule kuna kero za miundombinu ikiwamo vyumba vya kujistiri, mabweni, wanafunzi kutembea umbali mrefu huku wakiwa kwenye siku zao.

"Hebu tufikiriea mtoto anatembea umbali mrefu... tunaomba wabunge waangalie suala hili kwa mapana na kuangalia hata kwenye bajeti inayofuata ili kutolewa VAT ili kuwafikia watoto wengi,"alisema.

Kwa mujibu wa tafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu(NIMR), pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa hedhi mwaka 2019, asilimia 60 ya wasichana hawamudu gharama za taulo za kike huku asilimia 28 pekee ndio wenye uelewa juu ya hedhi salama.

# Waziri ataka kuwapo bima na mikopo wavuvi, wafugaji

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amezitaka taasisi za bima na za kifedha kuwakomboa wafugaji na wavuvi kwa kuwawezesha kuwa na bima ya kulinda vitega uchumi vyao ili wakopesheke.

Alisema hayo juzi akifungua kikao cha wadau wa dawati la sekta binafsi ambalo lipo chini ya wizara hiyo.

Alisema wafugaji na wavuvi wamekuwa wakikabiliwa na kero ya kutokukopesheka kirahisi na taasisi za kifedha na hivyo kuwafanya washindwe kuitumia fursa ya mikopo kukuza mitaji yao.

Naibu Waziri huyo alisema kutokana na hali hiyo Wizara imeona ni vema kuwakutanisha wadau kujadili na kupata suluhisho kwa wakulima na wafugaji kuwa na bima.

"Mifugo na samaki ni uwekezaji na ni biashara kubwa hivyo taasisi hizi za bima na fedha lazima ziwe na mtazamo huo na kwamba kufanya kazi na wafugaji na wavuvi kutawaletea tija pia,"alisema.

Alifafanua kuwa lengo ni kuhakikisha uwekezaji na biashara kwenye sekta za mifugo na uvuvi zinakua na mchango wake katika kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Alishauri taasisi za fedha kuangalia uwezekano wa kupunguza riba kwenye mikopo ili wafugaji na wavuvi wakopesheke kirahisi.

Kaimu Katibu Mkuu anayeshughulikia sekta ya Mifugo, Dk. Bedan Masuruli, alisema sekta za mifugo na uvuvi zinahitaji kuendelezwa na moja kitu kinachotakiwa ni mitaji.

Kwa upande wake, Mratibu wa Dawati la Sekta Binafsi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Michael, alisema dawati lilifuatilia upatikanaji wa bima kwa wafugaji ili kuwasaidia wafugaji na wavuvi kupata mikopo.

"Shirika la Bima la Taifa (NIC), limetoa bima kwa vyama vya ushirika vya wafugaji vitatu na vyama vya ushirika vya wavuvi vitatu,"alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Utafiti, na Maendeleo ya Masoko ya Bima Tanzania, Muyengi Zakaria, alisema wameshazielekeza kampuni zote za bima nchini waandae bidhaa ambazo zinakidhi mahitaji ya wafugaji na wavuvi.

# WB yatoa bilioni 300 uwekezaji TEHAMA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI ya Dunia (WB), imeipa serikali zaidi ya Sh. bilioni 300 kwa ajili ya kuboresha Teknolojia ya Habari ya Mawasiliano (TEHAMA) nchini.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk.Faustine Ndugulile, alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akifungua maonyesho ya utafiti na ubunifu yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), jijini hapa.

Alisema serikali inajipanga kuwezesha ubunifu na utafiti kwa vijana kuhusu masuala ya TEHAMA ili nchi iendelee kupiga hatua katika masuala hayo.

"Nchi imepiga hatua kwa kiasi kikubwa mambo mengine lazima sisi wenyewe tujisifie, miaka mitano iliopita katika nyanja ya TEHAMA na mifumo ndani ya nchi yetu tulikuwa tunaagiza nje ya nchi,tena kwa gharama kubwa na kulipia leseni na ukichelewa unafungiwa,"alisema.

Aliongeza: "Kati ya asilimia 70 mpaka 80 ya mifumo ambayo inatumika serikalini imetengenezwa na vijana wazalendo tunapaswa kujipongeza,"alisema Waziri.

Alisema serikali katika eneo hilo inahitaji kuweka nguvu kwa sababu vijana hao wanatakiwa kulelewa na mawazo yao ili kuhakikisha yanaingia sokoni.

"Vijana wanakuwa na mawazo, lile wazo ni biashara na ajira yenyewe ili bidhaa zao ziingie katika soko, lengo la serikali ni mpaka miaka mitano ijayo Tanzania inakuwa na wataalamu wengi katika nyanja mbalimbali za ubunifu, hata kama hatutaitumia sisi basi dunia inufaike na ubunifu wa vijana hawa,"alisema.

Alikitaka chuo hicho kushiriki katika ndoto za serikali za masuala hayo ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha ubunifu pamoja na utengenezaji wa bidhaa za TEHAMA.

"Hivi sasa vita haitapiganiwa ardhini kwa kushambuliwa na majeshi, bali inapiganwa katika mitandao,kupitia kompyuta na simu za

mkononi. Ni lazima tujipange kama nchi kuwa na uwezo wa kuzuia mashambulizi kama hayo katika maeneo ambayo tunahitaji,"alisema.

Makamu Mkuu wa UDOM, Prof. Faustine Bee, alisema chuo hicho kitaendelea kushirikiana na serikali katika masuala yanayohusu tafiti kwenye nyanja za utafiti,ubunifu na TEHAMA.

## Waziri ataka nguvu mpya ukombozi mtoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema jamii inatakiwa kujitafakari upya katika kukomesha udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto.

Dk. Saada alisema hayo juzi katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yalioandaliwa na Jumuiya ya Kumwendeleza Mtoto wa Kike Zanzibar (FAWE) yaliyofanyika katika Ukumbi wa Shekh Idris Abdulwakil, Kikwajuni.

Alisema umefika wakati kwa jamii kufahamu uzito wa suala hilo linavyoathiri jamii hasa watoto ambao ndio viongozi wa baadaye na kurudisha nyuma juhudi za maendeleo nchini.

Waziri Saada alisema ni wakati sasa kutafakari na kulisimamia jambo hilo kwa pamoja katika kutokomeza ukatili wa watoto ikiwamo unyanyasaji.

Alisema mambo hayo yalikuwa yakipingwa zamani lakini hivi sasa yanajitokeza na kushika kasi kwa kuwaharibu watoto kisaikolojia na kuwaharibia malengo yao ya baadaye.

"Tunasherehekea ukombozi wa mtoto wa Afrika lakini bado tuna wimbi ambalo limetukaba ndani ya taifa letu. Tushirikiane katika kulipiga vita jambo hili kwa manufaa ya vizazi vyetu vya sasa na baadaye," alisisitiza.

Alisema ni vyema kwa jamii kumuondolea mtoto woga pale hali ya hatari inapomkabili ili kujilinda wakati wote.

Kuhusu Siku ya Mtoto wa Afrika, alisema inawapa muda kutafakari majukumu yao katika kutimiza ndoto zao katika kupata fursa za kielimu, kisiasa, kijamii, kiuchumi na kusimamia kupata haki zate zinaowahusu.

Aidha, alisema wanawake wanahitaji kutambulika na msaada na wanawake wengi wamejikita katika uchumi wa buluu kwa kujiajiri wenyewe bila ya kutegemea ajira kutoka serikalini.

Mwenyekiti wa FAWE, Dk. Mwatima Abdalla, alisema ili jumuiya hiyo izidi kufanikiwa katika kuwasimamia watoto, kuna haja kwa serikali kuendelea kuiunga mkono katika suala la misaada kila inapohitajika.

Pia alisema FAWE inajikita katika kuwafunza vijana kujiajiri wenyewe kupitia malighafi iliyokuwepo katika maeneo yao lengo ni kuona Zanzibar haiagizi vitu ikiwemo sabuni, mafuta na vitu vyingine ambavyo vinatengezwa nchini.

# Karume: Kustaafu si mwisho wa maisha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, amesema kustaafu si mwisho wa maisha bali ni kufungua ukurasa mpya wa maisha ambayo huenda yakawa mazuri zaidi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wafanyakazi wastaafu na wanaotarajiwa kustaafu kutoka taasisi mbalimbali za serikali za Zanzibar na Tanzania kwa ajili ya kuzifahamu fursa zinazotolewa na benki ya CRDB ili kujikwamua kimaisha.

Karume aliwataka watumishi wa serikali wanaostaafu kuondoa hofu kwa sababu kustaafu hakumaanishi kwamba ni mwisho wa maisha na kwamba watu waache imani potofu kwamba kustaafu utumishi wa serikali maana yake ni kwenda kuishi katika maisha magumu. Aliwataka watumishi wanaotarajiwa kustaafu kujipanga mapema na kutafuta fursa zitakazowawezesha kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kuingiza kipato cha ziada.

"Nimefurahishwa na mipango yenu benki ya CRDB ya kuwaita watumishi wanaotarajiwa kustaafu lakini na sisi wafanyakazi tuliostaafu kwa ajili ya kutupa elimu ya fursa mbalimbali zinazopatikana katika benki hii," alisema. Aidha, alisema utafiti unaonyesha ifikapo mwaka 2030 asilimia 16 ya watu watakuwa wale waliofikisha umri wa miaka 60 ambao watakuwa tayari wamestaafu utumishi wa umma.

Naye Ofisa Mkuu wa Biashara kutoka CRDB, Joseph Witts, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wastaafu wanajengewa mazingira mazuri yatakayowahakikishia maisha bora.

Alisema benki imefunguwa akaunti maalumu ya "Thamani akaunti" ambayo ni mahususi kwa ajili ya wazee ambayo huwapatia faida itakayowanufaisha.

Aidha alisema wamefungua 'akaunti ya wastaafu' ambayo hupokea mafao yao katika mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii waliyokuwa wakiwekewa fedha zinazotokana na mishahara.

"Wazee wastaafu na wanaotarajiwa kustaafu itumiyeni benki yenu ya wazalendo kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi changamoto mbali mbali zinazowakabili wazee wastaafu"alisema.

Baadhi ya wastaafu waliohudhuria mkutano huo, walielezea kufurahishwa na mipango mizuri ya benki hiyo ambayo imelenga kuwasaidia wastaafu kuona kwamba wanapata matumaini ya kuishi vizuri.

Balozi Silima Ame Pereira, alisema amefurahishwa na mipango iliyobuniwa na CRDB ambayo imelenga kuwasaidia wastaafu na kuwashika mkono kuona wanaendelea na matumaini ya kuishi kwa mafanikio.

"Nimefurahishwa na mikakati ya benki ya CRDB ambayo imelenga katika kutusaidia sisi wazee na kutuonyesha njia ya kuishi kwa matumaini makubwa," alisema.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akitoa hotuba ya kuahirisha mkutano wa tatu wa baraza la kumi la wawakilishi huko Chukwani, Zanzibar juzi jioni. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar, Uswisi kushirikiana vita dhidi ya rushwa, uhujumu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali itaendelea kushirikiana na Uswisi katika kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa rushwa na uhujumu uchumi itakayoisaidia serikali kuandaa mbinu bora za kupambana na wahusika wa vitendo hivyo.

Akizungumza na Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Didier Chasot, aliyefika ofisini kwake Migombani, Zanzibar, kwa ziara yake yenye lengo la kukuza uhusiano wake na Zanzibar, Othman alisema serikali imeandaa mfumo huo kwa lengo la kuhakikisha Zanzibar inaendelea kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa pamoja na kuzuia matumizi ya mali zinazopatikana kwa njia haramu.

Alisema mfumo huo umekuwa ukitumika katika nchi mbalimbali duniani ambao umekuwa chachu ya kupambana na tatizo hilo hali iliyopelekea kuendelea kwa nchi hizo.

Pia alisema Uswisi imeingia makubaliano na Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Zanzibar (ZAECA) kwa ajili ya kujenga uwezo katika kuzifuatilia mali za watu waliopatikana na hatia ya uhalifu chini ya sheria zinazoambatana na rushwa na uhujumu uchumi.

Kuhusu utawala bora, Othman alisema serikali imejipanga katika kujenga uwezo wa taasisi mbalimbali na kutoa mafunzo kwa watendaji wa taasisi hizo pamoja kuandaa mpango wa urekebishaji wa baadhi ya sheria zinazohusika na usimamizi wa masuala mbalimbali nchini.

Naye Balozi Chasot alisema nchi yake itaendelea kuisaidia Zanzibar katika kuhakikisha sekta za afya, utawala bora na tatizo la ajira kwa vijana linapungua nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
DANI
TELE
JUMAMOSI JUNI 19, 2021



DAYNA NYANGE ASANTE Uk.14




ZUCHU ASAKWA

# Wimbo wake wateteresha ndoa

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Zuchu, wiki hii ametambulisha ngoma yake mpya inayoitwa 'Nyumba Ndogo, ' ambayo licha ya kuwa tishio, umesababisha hisia mchanganyiko katika jamii.

Wimbo huo wenye maadhi ya Singeli na Mchiriku, ujumbe wake umewakanganya mashabiki wengi hasa wanawake walio katika ndoa.

Zuchu katika wimbo huo anasimama kama mwanamke mwenye tabia ya kuchukua waume za watu, na bila kupepesa macho anajisifia na kujitambulisha kwa kujiamini kwa mke wa mwanamume anayejivinjari naye kuwa yeye ni nyumba ndogo wake.

Maneno yaliyomo ndani ya wimbo huo kama vile kuhalalisha kimada au nyumba ndogo ni kama fasheni kwa wanawake, yameibua malalamiko kwa baadhi watu ambao wanasema ni kwenda kinyume na maadili ya Kitanzania.

Mwajabu Saidi, mkazi wa Temeke jijini Dare s Salaam, amesema licha ya wimbo huo kuwa mzuri, lakini ujumbe wake ndio wenye kuleta ukakasi, hasa kwa vijana wanaotamani kudumu katika ndoa zao.

"Zuchu ni msanii mkubwa na kila kitu anachokisema katika wimbo wake ni ujumbe tosha katika jamii, hili la kuhalalisha nyumba ndogo na kuonekana kama ni jambo la kawaida anaweza kuwapotosha wasichana wakiamini kuwa na mume wa mtu ni sehemu ya maisha," amesema.

Amesema wanawake walio kwenye ndoa zao, wamekatishwa tamaa kutokana na wimbo huo wa Zuchu.

"Sijui kama watafurahishwa nao kuusikia, mume anauma sana si kama wasioingia kwenye ndoa wanavyofikiria" ameongeza

Christina Japhet, kwa upande wake amesema haoni tatizo na wimbo huo, kwani Zuchu ni msanii na anauwezo wa kuumba maneno ya kisanii ili kufikisha ujumbe wake.

"Mimi sioni tatizo wanaomkosoa watakuwa wanamuonea tu, unajua kila mwimbaji anatafuta maneno kwa ajili ya kupata mashabiki. Kusikifia nyumba ndogo si kama kapotoka kimaadili bali amekua kisanii na anaonyesha kipaji chake ya uimbaji," amesema Christina.

BASI SAWA

# Mzee Sumaku azidiwa majonzi



NI Majonzi mazito yanaendelea kuwakumba waigizaji wa vichekesho vya Mizengwe, huku Mzee Sumaku, akionekana kuzidiwa zaidi kutokana na baada ya marehemu Mzee Matata, kuwa kama mmoja wa familia yake.

Mzee Sumaku, amesema jambo linalomuumiza sana ni kitendo cha Mzee Matata, kumhusia kuitunza familia kabla ya kifo chake.

"Matata na mimi ni zaidi ya ndugu, mara ya mwisho tulikuwa Temeke Hospitali alipozidiwa aliinita mbele ya mkewe, akaniambia nikifa familia yangu nakuachia wewe naomba unilelee wanangu kile kitu kiliniuma sana, nilijaribu kumpa nguvu ila nilishajua anaashiria nini, tayari aliona haponi" amesema Mzee Sumaku

Mzee Matata alikuwa ana jumla ya watoto wanne na mke mmoja.

# Fid Q ambariki Nandy kipekee



RAPA kutoka kundi la Weusi, Fid Q, amesema katika tasnia ya muziki nchini, kuna wanawake wachache wanaotamba na kukubalika na mashabiki.

Amesema Nandy ni mmoja wa mwanamuziki wa kike mwenye mafanikio na ni lazima wasanii wa kiume kuwasaidia ili kutimiza malengo yao.

"Ukweli ni kwamba tuna wasanii wachache wa kike wenye mafanikio, ni muhimu kuwasaidia ili wawe wakubwa na kutimiza ndoto zao," amesema Fid Q



# Dayna Nyange asante

KATIKA kile kinachoonekana kwamba Dayna Nyange, hana utani, amedondosha EP yake na kueleza sasa ni mwendo wa kimataifa.

EP hiyo ambayo inaitwa 'Elo' jina litokana na wimbo aliomshirikisha Davido kutoka Nigeria, inatarajiwa kufanya vizuri kutokana na nyimbo tamu zilizokuwamo ndani.

Baadhi ya nyimbo zinazopatikana ni Teketea, Shona, Maujuzi na Elo ambayo ilitoka Mei 28, mwaka huu.



# Joshen 'Giny' aachia 'Wataachana' kibabe

MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi Joshen Adam, maarufu kama 'Giny' ameachia ngoma yake mpya inayoitwa 'Wataachana' ambayo imeanza kuwatikisa mashabiki.

Meneja wa msanii huyo, Njei BM, amesema wimbo huo ambao unapatikana kwa mfumo wa Audio, umerekodiwa Asset Studio, chini ya Prodyuza Kazzu Beats, na utatambulishwa rasmi hivi karibuni katika vituo mbalimbali vya redio.

"Wimbo huu 'Wataachana' umeleta ushindani wa kimuziki na kuonyesha jinsi Giny anavyofikiria kuwaridhisha mashabiki wake, tunawaomba sana kusikiliza katika mtandao wa You tube na hivi karibuni tutauzindua rasmi katika vituo vya redio," amesema Njei BM.

# Makuka tutamkumbuka kwa hizi...

**Na Adam Fungamwango**

MAKUMBELE ni wimbo maarufu sana nchini ambao ulipigwa na bendi ya Maquiz Original. Ulikuwa ni utunzi wake hayati Kaumba Kalemba mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Mmoja wa walioshiriki kwenye wimbo huo, akipiga gitaa la rythm, Omari Makuka, amefariki dunia.

Makuka alifariki dunia Juni 8, mwaka huu, Dar es Salaam. Mwanamuziki hiyo aliyekuwa akiishi Mtaa wa Aggrey, Kariakoo alizikwa Juni 9, kwenye Makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam, msiba ukiwa kwa mtoto wake Ukonga Sitakishari.

Mwanamuziki huyo, atakumbukwa kutokana na mchango wake mkubwa kwenye tasnia ya muziki, akihudumu bendi mbalimbali kama Super Matimila, Maquiz Original, Uda Jazz na MK Group.

Mwanamuziki huyo alikuwa na uwezo mkubwa wa kupiga gitaa la solo, second solo, ambalo kwa wanamuziki wa Congo DR, wanalitambulisha kama mini solo na gitaa la rhythm.

Kwenye safu hii tutaangalia baadhi ya nyimbo maarufu ambazo ameshiriki.

**NATOA ONYO-SUPER MATIMILA**

Ni wimbo ambao ulitungwa na Dk. Remmy Ongala mwanzoni mwa miaka ya 1980 ambao unawaonya wale kwenye tabia ya kupenda wake na waume za watu. Wanaambiwa kuwa mke wa mwenzio usimvalie koti, wala mume wa mwenzio usipakalie wanja. wenye tabia hiyo wanaonywa, mkuki mtamu kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu. Makuka alipiga rhythm kwenye wimbo huo.

**ALIMASI-SUPER MATIMILA**

Kwenye wimbo huu pia marehemu, Makuka alipiga gitaa la kati, rhythm. Ulikuwa utunzi wake marehemu Kasaloo Kyanga mwanzoni mwa miaka ya 1980 na ukiusikiliza wimbo huu kuna sehemu mtunzi alinogewa na wimbo na kupiga kelele 'Makuka Yee'. Ni wimbo unamhusu mwanamke anayemlalamikia mume aliyemtelekeza na watoto na kusababisha kuishi kwa tabu.

**SAKINA-UDA JAZZ BAND**

Huu ni utunzi wake mwenyewe Omari Makuka na yeye mwenyewe kupiga gitaa la solo. Hapa alikuwa kwenye bendi ya Uda Jazz akiwa kama kiongozi wa bendi.

Ni wimbo unaomzungumzia binti mmoja denti Sakina ambaye badala ya kwenda shule anakwenda kufanya starehe. Anatoka na nguo za shule, akifika huko anabadilisha, shati la shule anatia kwenye mkoba wa shule na kuvaa la ndege. Ni mashati ambayo katikati ya miaka ya 1980 yalikuwa maarufu sana na yalivaliwa na wajanja na watoto wa mjini tu.

**MAKUMBELE-MAQUIZ ORIGINAL**

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, Maquiz Original ilitoa kibao kilichotokea kupendwa sana, 'Makumbele'. Ni utunzi wake marehemu Kaumba Kalemba. Hayati Makuka alikuwa ameshalipa kisogo kundi la Uda Jazz na kuhamia bendi hii. Kwenye wimbo huu alipiga second solo au mini solo, gitaa ongozi la solo likipigwa na Dekula Vumbi Kahanga.


Ni wimbo ambao mwanamke amevumilia mengi kutoka kwa mumewe, lakini sasa ameshindwa na kufika mwisho.

**MAUMIVU MAKALI-MK GROUP**

Ni wimbo mkali sana ambao ulitungwa pia mwanzoni mwa miaka ya 1990, Makuka akiwa amejiunga sasa na bendi ya MK Group 'ngoma ya magharibi,' wakati huo wakipiga New Africa ghorofa ya saba.

Wimbo huu ulitungwa na aliyepiga solo kwenye wimbo huo, marehemu Joseph Mulenga, marehemu Makuka akipiga rhythm.





# Simbinlani Shujaa;Haramu kwako, kwetu halali

**Na Adam Fungamwango**

SIMBINLANI Shujaa ni filamu inayotufundisha kila mmoja kuheshimu hisia za mwenzake. Kuna kitu ambacho kwako kinaweza kuwa si kizuri, lakini kwa mwenzako hakina tatizo, basi mwache tu. Haiwezekani kitu ambacho kwako hukipendi, basi ulazimishe watu wote wakikatae kama wewe.

Imechezwa na wasanii Anita Ngereza, Agnes Makalla, Ayoub Kinyamagoha, Jesco Maryego, Madaraka Manase, Enea Msukwa, Haidari Mlingo, Sakina Njoka na wengineo.

Ndani ya himaya fulani, mfalme anafariki. Baada ya msiba kumalizika anamuachia urithi kijana wake wa kiume.

Tofauti na baba yake aliyetawala kwa busara, mfalme huyo kijana anatawala kwa mkono wa chuma.

Wananchi hawana amani. Kwenye himaya hiyo kuna kijana mmoja aitwaye Simbi. Ni kijana mwenye nguvu, busara na anayependwa na wengi. Dada wa mfalme kijana anatokea kumpenda Simbi. Awali Simbi alikataa. Lakini alipotaka kujiua akakubali. Penzi halijaribiwi. Simbi akaanza kumpenda Zao.

Penzi halina siri na siri si ya watu wawili, Mfalme akagundua. Akampiga mkwara dada yake asiendelee kuwa na uhusiano na Simbi, kwani ni kijana wa kimaskini na dhalili. Akamwambia atamuozesha kwenye himaya nyingine ya mfalme. Zao akakataa. Akamwambia moyo wake uko kwa Simbi.

Kijana mfalme akaamua kuitesa familia ya Simbi pamoja na yeye mwenyewe. Kazi yake ikawa ni kutuma walinzi wake watiifu kwenda kutesa dada za Simbi, pamoja na yeye mwenyewe.

Hali ilizidi kuwa mbaya, lakini Zao na Simbi hawakuacha kupendana. Ilikuwa ni kama kumpigia gitaa mbuzi. Mfalme naye hakukoma, aliwaandama kweli kweli. Dada wa mfalme uzalendo ulimshinda na kuamua kujiua. Lilikuwa pigo kubwa na mfalme. Kwa hasira akawasingizia Simbi na dada zake wawili ndiyo waliosababisha dada yake ajiue. Pamoja wazee wa kimila kudai hakuna ushahidi wa kuwatia hatiani, mfalme hakuridhika, akataka kuwaua mwenyewe kwa upanga wake.

Ndipo mzimu wa dada yake, Zao ulipotokea wakati panga lipo juu kutaka kukata kichwa cha Simbi, ukazuia. Mfalme alichanganyikiwa na kukubali kuwa alifanya makosa kutosikiliza hisia za dada yake.



# Simi kitumbo kinawaumbua wengi

MWIMBAJI wa Nigeria, Simi amekanusha uvumi ulioenea mitandaoni kwamba ana ujauzito wa mtoto wake wa pili.

Simi ameandika katika ukurasa wake wa Instagram, kuwa yanayozungumzwa juu yake ni uongo kwani kwa sasa anawajibika kumlea mtoto wake.

Tamko lake hilo lilitokana na baadhi ya mashabiki wake kuhoji kama kweli ana ujauzito na anatarajia kumpata mtoto wa pili hivi karibuni.



## Baba Ijesha utasota rumande

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Olanrewaju Omiyinka, maarufu kama Baba Ijesha, ataendelea kusota rumande baada ya kunyimwa dhamana.

Baba Ijesha amewekwa kizuizini tangu Aprili 22, mwaka huu, baada ya polisi wa jimbo la Lagos, kumkamata na kumfikisha mahakamani kwa kosa la kumlawiti msichana wa miaka 14.

Staa huyo wa filamu alifikishwa mbele ya mahakama ya Yaba, siku ya Jumatano, na baada ya kusomewa mashtaka hakimu alimkatalia dhamana.

Tukio hilo liliibuliwa na mchekeshaji maarufu nchini Nigeria, Princess, ambaye alilalamika binti yake kunyanyaswa kingono na Baba Ijesha akiwa nyumbani kwake.

## Travis kama unampenda, mbona ulimuumiza?

MWANAMUZIKI wa kufokafoka wa Marekani, Travis Scott, ameweka wazi kuwa bado anampenda mzazi mwenzake Kylie Jenner, licha ya kuachana mwaka mmoja uliopita.

Staa huyo ambaye aliambatana na mama wa mtoto wake, Kylie, amesema kuachana kwao si kwamba wao ni wapinzani, bali kutoka moyoni mwake bado anampenda.

"Nakupenda, nakupenda," alisema Scott.





## Drake hakamatiki tena

RAPA mkali wa Marekani, Drake, amezidi kupasua anga baada ya rekodi yake kuwashangaza watu wengi.

Hivi karibuni, Drake ameweka rekodi mpya baada ya kutambulika ni msanii pekee wa muziki wa Hip hop ambaye ametokeza mara nyingi katika chati kubwa za muziki duniani.

Katika nyimbo 100 za Billboard, Drake ameingiza maingizo 233, akifuatiwa na Lil Wayne (173), Future (123)Nicki Minaj (118) na namba tano ni Kanye West mara 109.

## Gwen unataka kuwanyima pilau wenzio

IMERIPOTIWA kwamba mwimbaji Gwen Stefani na mchumba wake, Blake Shelton, wanafanya mpango wa kuoana kwa siri.

Kulingana na mtandao wa PageSix, walionekana wawili hao wakiwa na mama wa Shelton katika ranchi ya Santa Monica, California nchini Marekani.

Chanzo kimoja kimesema 'kapo' hiyo imeandaa eneo maalum ndani ya ranchi hiyo kwa ajili ya sherehe ya harusi.



MAKALA

# KKKT Kijitonyama inapoonyesha njia teknolojia ibada mtandaoni

**Na Anaeli Mbise**



Mchungaji kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, akihubiri katika moja ya ibada zinazoendeshwa kwa njia ya mtandao. **PICHA MTANDAO.**

MATUMIZI ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) hususani kompyuta na intaneti yanakuwa kwa kasi kubwa duniani na hapa nchini.

Shughuli nyingi za uendeshaji wa ofisi, kama vile kuchapa taarifa mbalimbali, mawasiliano na hata kuhifadhi nyaraka na taarifa hizo zinafanywa kwa kutumia TEHAMA.

Hali hii inadhihirishwa na ripoti ya kupima mawasiliano katika jamii ya 2018 ambayo ilikuwa na mapendekezo ya namna ya kuwekeza katika teknolojia kunavyoleta mabadiliko ya kidijitali kimataifa na kuwezesha watu kufikia huduma mbalimbali kwa njia rahisi.

TEHAMA kwa sasa imebadilisha pia hali ya upatikanaji wa taarifa na habari kuwa haraka na rahisi tofauti na miaka ya 1960, hadi kufikia 2000 ilipoanza kushika kasi.

Tangu kuzuka kwa ugonjwa wa corona, viongozi, taasisi na masharika mbalimbali wamekuwa wanatumia teknoliji hii kuwasiliana na hata sehemu za ibada kama misikiti na makanisa nayo mahubiri yamekuwa yakiendeshwa kwa njia ya mtandao ili kuwafikia waumini walio wengi.

Moja ya kanisa ambalo limekuwa na matumizi ya TEHAMA katika mahubiri ni Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Katika dayosisi ya mashariki na Pwani, usharika wa KKKT Kijitonyama, ni mmoja kati ya sharika ambazo teknolojia hii imekuwa kwa kasi na kuleta mapinduzi makubwa ndani na nje ya kanisa kwa waumini wanaofuatilia ibada za kila Jumapili pamoja na masifu ya asubuhi na jioni.

Mchungaji kiongozi wa usharika huo, Dk. Eliona Kimaro, anasema kuwa alianza ibada za mtandaoni kwa kuanzisha televisheni ya youtube akiwa usharika wa Kariakoo mnamo 2012.

"Ni yangu kubwa ilikuwa ni kufikia maeneo ya misoni kwasababu tulikuwa na washarika wetu ambao walikuwa ni mabaharia wanakaa kwenye bahari wakati mwingine miezi mitatu mpaka sita pia tulikuwa na washarika wetu wanajeshi walipelekwa Congo na Somalia kwa hiyo wakati wa likizo wakawa wanauliza namna ambavyo watapata ibada kwa hiyo tukaanzia hapo kuwa na ibada za mtandaoni," anasimulia Kimaro.

"Tulijikuta tunahudumia watu walio ndani na nje ya usharika lakini pia wafanyabiashara wa Kariakoo walikuwa wanaenda China, Dubai India kwa ajili ya biashara na walikuwa wanakosa ibada huko ndipo tukaanza kwa lengo ya wao kupata," anasema Kimaro.

Mwaka 2017, alipohamishiwa na dayosisi usharika wa Kijitonyama alikuta kanisa hilo likiwa na ibada za mtandaoni, lakini anasema imekua kubwa zaidi kwa kuwa na huduma za kipaimara mtandaoni, maombi ambayo yanajulikana kama 'World Prayers Online' (WPO) pamoja na huduma za ibada.

Kwa kushirikiana na uongozi mzima wa kanisa hilo, Dk. Kimaro anasema wameundwa kamati maalum ya wataalam wa TEHAMA ambayo kazi kubwa ni kuendesha na kurusha shughuli za ibada.

Mch. Dk. Kimaro anakiri kuwa haikuwa kazi rahisi kwa jambo hilo jipya kupokewa kwa haraka kama hilo la ibada za mtandaoni, lakini anasema kuwa sharika zingine kama vile Kimara, Temboni, Mbezi Beach, Mbezi Luis pamoja na Boko zimekuwa nazo na ibada za mtandaoni.

"Ibada hizi za mubashara kupitia mtandaoni zilishika kasi wakati wa kipindi cha corona kutokana na marufuku ya watu wengi kutotoka nje na kwenda kwenye ibada na hivyo kuabudu kupitia mtandaoni ndipo umuhimu wa ibada za mtandaoni ikawa inafikia watu wengi," anasema Mch. Dk. Kimaro.

Katika kufanikisha ibada hizi mubashara katika usharika huo, Mch. Dk. Kimaro anasema kuwa watumishi mbalimbali wamekuwa wanatoa huduma za kimisionari ili kukidhi haja ya kuwafikia watu walio wengi.

Anataja baadhi ya watumishi ambao wamekuwa wanahudumu ni kama vile Mch. Denis Kalipi kutoka Kongo, Mwal. Tumainiel Mbwambo, Godluck Mushi, Renald Mlawi, Musa Musa, Elirehema Pallangyo, pamoja na Emanuel Shemdoe.

TEHAMA pia anasema imesaidia kuzindua huduma ya maombi kwa njia ya mtandao ambayo yanajulikana kama 'World Prayers Online' ambalo lilikuwa ni wazo la kichungaji kutokana na watu walio wengi kuwa na uhitaji wa maombi.

"WPO imeanza kutokana na watu kuhitaji neno la faraja wamelazwa hospitali India, Canada, Uingereza, India na wengine walikuwa hawana kazi. Huduma hii ni ya masaa 24 kwa kutumia namba za simu na wahudumu wa kiroho wanatoa huduma," anasema.

Mtaalam wa TEHAMA ambaye pia ni mzee wa kanisa Michael Kejo, anasema miundombinu ya mitambo pamoja na vifaa vya kurusha ibada hizo mubashara zimegharimu zaidi ya Milioni 530.

Anasema kukua kwa ufanisi wa TEHAMA, ni kutokana na ushirikishwaji wa waumini pamoja na uongozi madhubuti wa kanisa ukiongozwa na Mchungaji Kimaro.

"Kutokana na wingi wa watu ndani ya kanisa hilo kuna mahema mawili upande wa kushoto na kulia na kila upande una screen sita za kuonyesha ibada mubashara na hii inasaidia watu wenye ugonjwa wa kisukari, lakini ni kuwafanya watu wasijisikie wapweke wakiwa kanisani na tunao watu zaidi ya 80,000 wanaofuatilia ibada za mtandaoni kwa sasa," anasema Kejo.

Vijana ambao ni washarika wa kanisa ndiyo ambao wanarusha ibada hizo mubashara kwa kupangiana zamu, lakini pia wapo wanaokuwa wamemaliza vyuo na huwa wanajifunza vitu kimatendo zaidi kuliko nadharia.

Uanzishwaji wa ibada za mubashara katika kanisa hilo umesaidia pia wanafunzi wanaosoma masomo ya TEHAMA kujifunza kimatendo zaidi pamoja na tafiti.

"Katika kanisa hili kuna wanafunzi wengi huwa wanakuja kujifunza kimatendo pia kuna Mchungaji mmoja anaitwa Kurwa Sadataley, ambaye anasoma chuo cha Sauti Mwanza shahada ya uzamivu katika masuala ya TEHEMA, hii ni faida kubwa maana watu wanajifunza," anasema.

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, anaunga mkono hoja ya ibada hizo kurushwa mubashara kwa njia ya mtandao, huku akisema teknolojia hiyo imechelewa kutumika katika makanisa.

"Ni jambo jema sana kwa ibada kurushwa mubashara kwa njia ya mtandao kwa maana ujumbe wa mahubiri unakuwa unawafikia idadi kubwa ya watu walio katika kuta nne za kanisa na ambao wako nje ya kanisa," anasema.

Anasema moja ya kazi kubwa iliyoko ni kuhakikisha makanisa yanakuwa na wataalam ambao wana ujuzi wa kurusha ibada hizo mubashara, lakini pia ziendeshwe katika utaratibu unaoeleweka na uchaji unaotakiwa.

Askofu Dk. Shoo anaongeza "Vijana wengi kwa sasa ndiyo watumiaji wakubwa wa mitandao na ndiyo shemu ya walio wengi ndani ya kanisa hivyo itasaidia wao kupata mahubiri kwa urahisi na itawafanya wazidi kukua kiroho, kiakili, kiuchumi na kijamii,".


# ‘Fibroids’ yawa janga jipya la kiafya kwa wanawake Waafrika

Na Christina Mwakangale

UVIMBE kwenye mfuko wa kizazi ‘fibroids’ ama ‘myoma’ ni tatizo jipya la kiafya linalokua kwa kasi duniani na kuwakumba kwa kiwango kikubwa wanawake Waafrika, sababu mojawapo ikitajwa kuwa ni rangi ya asili ya ngozi yao ‘melanin’.

Melanin ni rangi ya asilia ya ngozi, nywele na macho inayoleta tofauti baina ya viumbe hai wakiwamo watu kulingana na eneo wanapotokea duniani kwa mujibu wa Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Matilda Ngarina.

Anaeleza kuwa fibroids huwakumba zaidi wanawake Waafrika kuanzia umri wa miaka 30 hadi 40, na kwamba sababu inatajwa ni rangi ya ngozi, na kuongeza:“Hata ukienda Marekani weusi ndiyo hukutwa na fibroids, sababu inaweza kuwa melanin yetu tuliyonayo, lakini ni mtazamo wa kidunia kwamba sisi Waafrika hupata fibroids,” anasema bingwa huyo bila kutoa maelezo zaidi ya namna ngozi ya asili inavyochochea tatizo hilo.




Mji wa mimba ulio na uvimbe maeneo tofauti tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Dokta Ngarina ambaye pia ni Rais wa Chama cha Madaktari wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi Tanzania (AGOTA), anasema kati ya wanawake 10 wanaofika MNH kwa uchunguzi wa masuala ya uzazi, kati yao nane hubainika wana uvimbe kwenye kizazi baada ya kufanyiwa kipimo cha ultrasound.

Anasema matumaini ni kwamba asilimia kubwa ya wanawake wanaokutwa na uvimbe huo, hauna uhusiano na ugonjwa wa saratani kama ambavyo baadhi hufikiri.

Ni asilimia ndogo sana ya uvimbe ambao huwa ni chanzo cha saratani. Kwa asilimia 0.5 pekee ndiyo wanaweza kuwa na saratani tena ambao watakuwa wamefikia umri wa miaka 70 na zaidi, anasema.

“Kwa kipindi cha takribani miaka 20 tangu nilipoanza kufanya kazi hii, nilikutana na binti mdogo wa miaka 20, akiwa na uvimbe wa kilo tatu kwenye kizazi. Ninasema ni mdogo sababu ndiyo ametoka katika umri wa balehe hata hajaanza kupata watoto,” anasema Dk. Ngarina.

“Zamani tulikuwa tukiona wenye uvimbe huu ni wa umri wa kuanzia miaka 30 na kuendelea, hasa kwa wanawake ambao hawakujaaliwa uzazi, hivi karibuni miaka mitano au 10 tumeona wanaopata ni wenye umri mdogo, mabinti ambao wametoka kupevuka.”

### UVIMBE WENYEWE

Bingwa huyo anasema kwamba uvimbe ‘fibroids’ kwenye mji wa mimba, ni vivimbe vinavyoota popote katika kizazi ambacho kina sehemu kuu tatu na unapoota hukua kwa kasi tofauti na kwa ukubwa tofauti na kuleta madhara ikiwamo kutoshika mimba au mimba kuharibika.

“Uvimbe kwenye kizazi sasa ni suala linaloendelea kukua, pengine inaweza kuwa linatokana na kukua kwa ugunduzi na uchunguzi wake sababu wanawake wanafika hosptalini. Lakini kuna ongezeko la ‘fibroids’ kuliko zamani,” anasema Dk. Ngarina.

Anasema kizazi kinakuwa na uvimbe wa aina tofauti ingawa fibroids zimeongezeka na kwamba duniani takwimu zinaonyesha asilimia 90 ya wanawake wote wana uvimbe.

“Wanawake hawa kwa asilimia 90 wana uvimbe wa aina tofauti wengine kama punje ya karanga, ila wengine kilo hata tatu, tano hapo shida inakuja. Hatujui sababu ni nini. Tatizo ya uvimbe huu huota na kukua taratibu, hautogundua kama upo, umeanza lini, hadi uanze kukupatia dalili,” anasema bingwa huyo.

### MADHARA YA UVIMBE

Dk. Ngarina anasema iwapo mwanamke akishika mimba akiwa na uvimbe, kustahimili kwa ujauzito hadi kujifungua kutategemea uvimbe umekaa sehemu gani kwa kuwa walio wengi mimba huharibika na kwamba chakula chake huwa ni damu na iwapo sehemu ulipoota ukawa unapokea damu kutoka mishipa ambayo pia inapeleka damu kwa mtoto tumboni, mimba itatoka.

“Kwa ambao walibeba mimba na hadi mimba miezi tisa, tutawafanyia upasuaji ili kutoa mtoto na uvimbe,” anasema bingwa huyo na kwamba fibroids husababisha mwanamke kuishiwa damu na kuzuia uzazi iwapo atahitaji kupata mtoto .

“Damu ikiwa ndogo lazima moyo utapiga kwa kasi, utahangaika kwa kusukuma damu chache iliyopo. Hapo magonjwa ya moyo huweza kujitokeza, mwanamke anaweza akadhani ana tatizo la moyo kumbe chanzo ni anaemia,” anasema bingwa huyo.

Anasema iwapo uvimbe ukiendelea kukua na kuongezeka utasababisha mzunguko wa hedhi kubadilika kila mwezi, kutokana na damu kushindwa kutoka ipasavyo.

Anabainisha kuwa mama huyu atakuwa na maumivu sababu kwanza kizazi kimekandamizwa, kibofu na njia ya haja kubwa zimeminywa na ataishiwa damu na kuhisi kizunguzungu, dalili hizo na kero ambazo mwanamke atazipata zitamfanya afike hospitali na kubainika ana uvimbe.

Dk. Ngarina anasema uvimbe huwakumba wanawake waishio maeneo yote, mijini na vijijini, na kwamba mijini wagonjwa hugundulika mapema zaidi kutokana na elimu kuhusu huduma hizo kuwafikia haraka.

Anasema madhara makubwa ya uvimbe huo ni kuhatarisha uhai, kwa kuwa damu hupungua mwilini na huweza kusababisha kifo iwapo upasuaji kuundoa utachelewa kufanyika.

### DALILI ZA UVIMBE

Dokta Michael Mbete kutoka Chuo cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), anasema dalili za uvimbe kwenye kizazi zinaweza kuwa hedhi nzito inayochukua muda mrefu, hadi wiki moja na pia akataja kinamama wanaochelewa kubeba mimba husababisha mfuko wa uzazi kuwa na vivimbe vidogo vidogo.

“Unapokaa muda mrefu bila kupata mtoto ni sababu ya uvimbe kuota kwenye kizazi,” anasema Dk. Mbete na kushauri wanawake kufanya uchunguzi wa mara kwa mara kubaini matatizo ya uvimbe na kupata tiba.

### SABABU UVIMBE

Bingwa wa Magonjwa ya Kinamama na Uzazi MNH, Dk. Vincent Tarimo, anasema uvimbe kwenye kizazi, unasababishwa na mfumo wa maisha ambapo binadamu hivi sasa hahitaji kuzaa watoto wengi.


Sababu nyingine, bingwa huyo anasema ni tofauti kati ya uzazi mmoja hadi mwingine, yaani kukaa zaidi ya miaka miwili hadi mitano bila kupata mtoto mwingine .

Shirika la Afya Duniani (WHO), kuhusu uzazi kinashauri muda wa kuzaa mtoto mmoja hadi mwingine, kiwe miezi 24 au miaka miwili, anasema.

Mabadiliko ya mfumo wa maisha, ikiwamo kuchelewa kuzaa zaidi ya umri wa miaka 35 kwa wanawake, ulaji wa vyakula usiozingatia lishe, watu kutotaka kuzaa watoto wengi miaka ya hivi karibuni, kumechangia tatizo hilo, anasema.



# Jumuiya Kimataifa zaungana kumlilia Kaunda



Hayati Keneth Kaunda, enzi za uhai wake. **PICHA: BBC**

**New York,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, ameungana na nchi za Afrika, kuomboleza kifo cha Rais wa zamani wa Jamhuri ya Zambia, Kenneth Kaunda.

Aidha, Zambia imetangaza siku 21 za maombolezo ya kitaifa kufuatia kifo cha muasisi wa taifa hilo, Kenneth Kaunda, aliyefariki dunia juzi, akiwa na umri wa miaka 97. Zambia inamkumbuka Kaunda kama baba wa taifa na mkombozi wa Zambia.

Taarifa iliyotolewa na Msemaji wake, Stephane Dujarric, akijibu swali kuhusu kifo hicho wakati wa mkutano na waandishi wa habari, jana, mjini New York, Guterres alisema ameshtushwa na taarifa za kifo hicho.

Alisema ni wakati mgumu na pengo kubwa: Natuma salamu za rambirambi kwa familia ya Rais wa zamani, kwa Serikali na watu wa Jamhuri ya Zambia."

"Kama baba mwasisi wa taifa la Zambia, Rais wa zamani Kaunda alikuwa na mchango mkubwa katika kupanga mkakati wa baada ya uhuru wa nchi hiyo, kuelekea demokrasia ya vyama vingi na alikuwa mtu wa kujitolea kwa maslahi ya Afrika."

Aidha, serikali ya Zambia imeagiza bendera zipeperushwe nusu mlingoti na kupiga marufuku matukio yote ya burudani kwa heshima ya kiongozi huyo wa zamani aliyekuwa na haiba kubwa.

Rais wa sasa wa Zambia, Edgar Lungu, alisema Kaunda amefariki wakati ambao hawakutarajia, huku akimueleza kuwa kiongozi halisi wa Afrika.

Katibu wa Baraza la Mawaziri Simon Miti, alisema katika hotuba kwa umma kupitia runinga kwamba, Kaunda alikufa kwa amani muda wa nane na nusu alafajiri ya jana, katika hospitali ya jeshi ambako alikuwa akitibiwa tangu Jumatatu, wiki hii.

Kaunda alifahamika kama KK, ni kiongozi wa chama kilichoiongoza Zambia baada ya uhuru kutoka kwa utawala wa kikoloni wa Uingereza.

Makamu wa rais wa zamani wa Zambia kati ya mwaka 2001 na 2003, Enoch Kavinde: KK atakumbukwa na kila mtu, ndiyo, kila mtu nchini humu, marafiki na maduni, watu katika chama chake na vyama vingine, tutamkosa sana kwa kuwa alikuwa nyota iliyong'aa"

Raia wa Zambia pia walitoa hisia zao pia kuhusu kuondokewa na mwasisi wa taifa lao.

Manfred Mubita alisema Mungu alimtumia Kaunda kwa kiwango kikubwa sana, kiasi cha kuikomboa Zambia na kuileta nchi hiyo mahala ilipo sasa. "Hakutaka kumwaga damu, hakutaka kufanya kitu chochote kwa manufaa yake binafsi. Hakuwa mtu mwenye ubinafsi," aliongeza.

**AFRIKA KUSINI**

Afrika Kusini imetangaza siku 10 za maombolezo ya kitaifa kufuatia kifo cha Kaunda.

Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa alisema, "Kufariki kwa rais Kenneth Kaunda kumetusikitisha sisi kama Waafrikakusini. Tunainamisha vichwa vyetu kwa huzuni na simanzi kwa kuondokewa na kipenzi chetu baba wa uhuru na umoja wa Waafrika. Tumeungana katika majonzi na familia ya Kaunda, serikali na watu wa Jamhuri ya Zambia."

Chama cha African National Congeress (ANC), Afrika Kusini kilimueleza Kaunda kama kiongozi jabali wa vita vya ukombozi barani Afrika, huku Rais wa zamani wa Afrika Kusini Thabo Mbeki, akimueleza Kaunda kama mtu wa watu.

**TANZANIA**

Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ametangaza siku saba ya maombolezo kufuatia kifo cha mwasisi wa taifa la Zambia Kenneth Kaunda.

Katika taarifa Rais Samia, amemtaja Kaunda kuwa miongoni mwa viongozi mahiri na jasiri kuwahi kutokea barani Afrika.

"Wakati wa uhai wake Hayati Kaunda alitoa mchango mkubwa katika harakati za ukombozi akishirikiana na viongozi wengine, akiwamo Baba wa taifa Mwalimu Julius Nyerere", ilisema taarifa hiyo.

Uhusiano kati ya Tanzania na Zambia, ulitokana na uhusiano kati ya viongozi wa nchi mbili wakati wa harakati ya kupigania ukombozi wa Afrika.

Suala muhimu barani Afrika katika karne ya 20 lilikuwa ni iwapo kuna uwezekano wa kubuni aina mpya ya jamii.

Kenneth Kaunda nchini Zambia na Julius Nyerere nchini Tanzania waliamua mwelekeo wa nchi zao, na kufanyia majaribio wazo la kuwa na jamii moja isiyoegemea misingi ya ukabila miongoni mwa mambo mengine isipokuwa maendeleo katika mataifa yao.

Wazo la kuwa na aina mpya ya jamii, ambalo lilikuwa msimamo wa vijana hao wa Kiafrika, lilikuwa muhimu kwa maendeleo katika mabara mengine.

Kaunda alichapisha vitabu kadhaa vilivyoelezea fikra za ujamaa wa Afrika, ambayo ilifuatwa na viongozi wengine wa Afrika ikiwa ni pamoja na Kwame Nkrumah nchini Ghana na Nyerere nchini Tanzania.

**BOTSWANA**

Risala za rambirambi ziliendelea kutumwa jana kufuatia kifo cha Kaunda huku Rais wa Botswana Mokgweetsi Masisi, akiwelezea rais huyo wa zamani kama mpiganiaji wa ukombozi wa nchi wa hadhi ya juu kutokana na alivyojitolea kwa maslahi yasiyo nchi yake pekee, bali kwa mataifa jirani.

Alisema Kaunda alikuwa 'rafiki wa dhati wa Botswana wakati ilipokuwa inapitia kipindi kigumu' kutokana na mchango wake katika harakati za kupigania uhuru wa nchi hiyo.

Rais Masisi alitangaza siku saba za maombolezo kwa heshima ya marehemu na kiongozi huyo wa Zambia:

**NIGERIA**

Rais wa zamani wa Nigeria Olusegun Obasanjo, alimkumbuka Kaunda, kama mmoja wa viongozi wa mwisho waliopigania uhuru ambaye alijitolea kwa njia tofauti.

**UINGEREZA**

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, aliandika katika ukurasa wake wa twitter, akisema amehuzunishwa na taarifa za kifo cha Kaunda na kutuma risala za rambirambi kwa watu wa Zambia.

**AU**

Moussa Faki, rais wa kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU), alisema Kaunda alikumbatia sana umoja wa waafrika wote, akiiweka nchi yake katika hatari kubwa kwa kutoa mficho kwa mavuguvugu ya kupigania uhuru.

**KAUNDA NI NANI?**

Kaunda alizaliwa akiwa mtoto wa mwisho katika familia ya watoto wanane ya mchungaji wa kanisa la Presbyterian, Aprili 28, mwaka 1924 katika misheni ya Lubwa, Kaskazini mwa Zambia, wakati huo ikijulikana kama Rhodesia Kaskazini.

Kaunda alitawala Zambia tangu mwaka 1964, wakati taifa hilo la kusini mwa Afrika lilipopata uhuru wake kutoka kwa Waingereza, hadi 1991 na alikuwa mmoja wa wanaharakati waliojitolea zaidi Afrika dhidi ya Virusi vya UKIMWI.

Kaunda alichukuliwa kama mmoja ya watu wa mwisho kwenye kizazi cha mashujaa wa uhuru Afrika. Alitawala Zambia kuanzia mwaka 1964 hadi 1991.

Anatajwa kama mwanzilishi, shujaa wa ukombozi Zambia, alifariki dunia katika hospitali ya jeshi mjini Lusaka, wiki hii, baada ya kulazwa katika hospitali hiyo akitibiwa ugonjwa wa nimonia, mtoto wake Kambarage Kaunda, alisema.

Kaunda ameacha utambulisho wa kipekee barani Afrika kwa vazi lake linalofahamika 'Kaunda Suit', pamoja na utaratibu wake wa kushika kitambaa cheupe mkononi kama ishara ya amani.

**Imeandaliwa: Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Kwa Habari Motomoto usikose
Gazeti lako la
Nipashe kila siku

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NO. 51/2018(EXTENDED "J")**
**(Asilia shaurila jinai No.239/2017,Mahakama ya Wilaya yaMomba)**

**JAMHURI..............................MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**1.ALLY ABDALLAH ISSA.........MJIBU RUFAA NO.1**
**2.MICHAEL GEOGE MWANJALA...........MJIBU RUFAA NO.2**
**KWA BWANA: 1.ALLY ABDALLAH ISSA**
**2.MICHAEL GEORGE MWANJALA**
**POPOTE ULIPO -TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya Tarehe 24/06/2021 siku ya Jumatano saa 03.00 asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA,ukikosa siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26/5/2021.

**Z.D.Laizer**
**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MBEYA**

116316601

---

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NO. 03/2019**
**(EXTENDED "J")**
**(Asilia shauri la jinai No.4/2017,Mahakama ya Hakimu mkazi Mbeya)**

**JAMHURI..................MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**VICK KASHILILIKA......................MJIBU RUFAA**

**KWA BIBI: VICK KASHILILIKA**
**POPOTE ULIPO -TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya Tarehe 24/06/2021 siku ya Jumatano saa 03.00 asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA,ukikosa siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26/5/2021.

**Z.D.Laizer**
**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MBEYA**

116316701

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANI**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 72/2018**
**(Asilia shauri la jinai No.4/2017,Mahakama ya Wilaya ya Rungwe)**

**JAMHURI.....................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**1.MOSES MWIMBEGE KIBON..........................................MJIBU RUFAA**
**2.ISRAEL ANANGISYE..................MJIBU RUFAA**

**KWA : 1. MOSES MWIMBEGE KIBONA**
**2. ISRAEL ANANGISYE**
**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe 22/06/2021 siku ya Jumanne saa 03.00 asubuhi bila kukosa,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
ELEWA KWAMBA,Mkikosa kufika siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila ninyi kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 11 Mwezi June, 2021.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

116316901

---

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NO. 38/2019**
**(EXTENDED "J")**
**(Kutoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya,jinai No.68/2017)**
**JAMHURI...............................MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**ELIAS KAYOWA........................MJIBU RUFAA**
**KWA :**
**BWANA: ELIAS KAYOWA**
**POPOTE ULIPO -TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya Tarehe 24/06/2021 siku ya Jumatano saa 03.00 asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA,ukikosa siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25/5/2021.

**Z.D.Laizer**
**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MBEYA**

116316801

---

**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANI**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 69/2019**
**(Asilia shauri la jinai No.2/2018,Mahakama ya Hakimu mkazi Mbeya)**

**JAMHURI.....................M RUFANI**
**DHIDI YA**
**OSEPH JUMA KYANDO.................MJIBU RUFAA**
**KWA BWANA; JOSEPH JUMA KYANDO**

**POPOTE ULIPO -TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani Tarehe 22/06/2021 siku ya Jumanne saa 03.00 asubuhi bila kukosa,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
ELEWA KWAMBA,ukikosa kuhudhuria siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 11 Mwezi Juni, 2021.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

116317001

---

## KURUDIA TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO. LTD** tunarudia tangazo la mnada wa hadhara wa gari la mdaiwa Sugu, mali ya Ndugu **ABDIEL ALPHONCE MSHANA (TOYOTA LEXUS -T 161 AXF) -** Gari lipo katika yard ya Makumbusho.

Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo analodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 26/06/2021, mahali dhamana ilipo.

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.
Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**0715683777 / 0712670704 / 0713052578**
**Email: info@sepcoauctioneering.co.tz**

116318001

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TGS CO LTD** Imepoteza kadi yake ya **TRAILER** yenye usajili namba **T 954 CKW** Yenye chasiss namba **01110299** Kwa yoyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Rbna. DAR/CEN/RB/ 304138/2021.**

116317701

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TGS CO LTD** Imepoteza kadi yake ya gari aina yake dyapacca250d yenye usajili namba **T 718 AVT** Yenye chasiss namba **65223499** Kwa yoyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Rb na. DAR/CEN/RB/ 304138/2021.**

116317801

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TGS CO LTD** Imepoteza kadi yake ya gari aina yake new Holland yenye usajili namba **T 219 AYF** Yenye chasiss namba **n7af1346** Kwa yoyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Rb na. DAR/CEN/RB/ 304138/2021.**

116317901

---

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie**
**0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

# HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu, ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho. Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini. Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

# Aolewe au afe-**11**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Baba kasema kuanzia leo ukalale nyumbani hadi siku ambayo tunaondoka."

Ilikuwa ni sauti ya Bishada ikimwambia Denny, muda mfupi tu baada ya kutoka kwenye Ofisi ya Kijiji.

Baada ya kuona muda unapita, Bishada alitumwa kwenda kumuangalia mgeni na kama kuna lolote basi akawaambie.

Familia ya mzee Ngoma tayari ilishamuona Denny kama mkombozi wao, hivyo pamoja na wao kuonekana kulindwa, lakini pia na wao hwakutaka wampoteze au baya lolote limpate.

Alionekana ni kama masiya aliyekuja kuwakomboa, au kutatua matatizo yote yaliyokumbana nayo tangu nyuma. Kwa bahati nzuri walikutana njiani.

"Siyo kwangu tena?"

"Baba hatoweza kukwambia. Lakini amemwambia mama na mama kaniambia mimi. Baada ya kunusurika jana, baba amesema wewe ukae nyumbani hadi siku zetu tano zilizobaki za kuishi kijiji hapa."

"Sasa Bishada, hivi tayari mnapo kwa kwenda?"

"Sijui baba. Atakuwa amepata kijiji cha kuhamia."

"Kwa nini usikubali tu barua ili muendelee kuishi hapa? Unajua wewe ndiyo unayemfadhaisha mzee wako?" Denny alimwambia Bishada huku akiwa amemshika mkono wakielekea nyumbani.

"Sitaki. Barua zote nimezikataa. Kama kuhama na tuhame tu."

"Kuna barua ambayo ikija utaikubali?"

"Mwanzo sikutaka barua yoyote, ila kwa sasa kuna nafasi ya mtu mmoja ambaye mpaka sasa hajaandika barua." Bishada alisema huku kimtazama Denny kwa wizi.

"Akiandika?"

"Hiyo ndiyo naisubiri."


"Nitaandika."

*************************

Ilikuwa ni siku iliyosubiriwa kwa hamu. Si kwa Bishada tu, bali hata baba na mama yake.

Ni baada ya Denny kuandika barua. Barua ya posa ikiomba ridhaa ya kumuoa Bishada.

Siyo kama hakuwahi kuandikiwa barua. Ziliandikwa lukuki. Tatizo ilikuwa ni kukubaliwa.




Bishada alikuwa akikataa barua za wanaume. Mzee Ngoma na mkewe walikuwa na uhakika kuwa sasa binti yao anaweza kukubali.

Ni kwa sababu kipindi kirefu alionekana kuwa na mgeni Denny au Denis.

Tangu walipomruhusu akae nyumbani hapo kwa ajili ya kile walichoona ni ulinzi, waliona kabisa binti yao alikuwa na furaha na amani.

"Nakubali." Alijibu baada ya kuulizwa na wazazi wake kama atakubali kuolewa na Denny.

Denny alikuwa ameandika mwenyewe barua na kumpa Bishada aipeleke kwa wazazi wake.

Ingawa aliishi kwenye nyumba ya kina Bishada, lakini alipewa chumba kimoja, huku Bishada akiwa kwenye chumba kingine.

Mara nyingi mchana, Denny na Bishada wamekuwa wakiwa pamoja. Wakitembea pamoja na kurahia maisha wakiwa pamoja.

Wala haikuhitaji ramli ya mganga wa kienyeji kuonyesha kuwa wanapendana na chochote kinaweza kutokea.

Kijiji kizima kilijua hivyo. Kuna watu wengi walioumia nafsi zao. Kijana mmoja kutoka mjini kuja kijijini kuwachukulia mrembo wao.

Mrembo aliyekuwa wakihitajiwa si na wanaume wa kijiji hicho tu, bali hata vijiji jirani.

Msichana aliyewatoa udenda vijana na wazee. Baadhi ya wanawake hasa wenye waume walifurahi kuona hali hiyo, kwani walikuwa na uhakika sasa wa waume zao kutulia.

Walikuwa na wasiwasi sana na ndoa zao juu ya msichana huyo. Baadhi ya wasichana nao walikuwa na hofu ya kutoshwa na wapenzi wao kwa sababu ya Bishada.

Kwao Denny alikuwa kama mkombozi. Sasa walikuwa na amani.

Tatizo lilikuwa walioumia kumkosa Bishada walikuwa na nguvu sana kuliko hawa wa upande wa pili.

Bishada kwa muda mfupi tu alitokea kumpenda Denny. Si kwa sababu alimuokoa yeye na familia yake kudhuriwa na watu wabaya kijijini kwao, lakini pia haiba yake, upendo, kujiamini na jinsi alivyomhemu.

Denny pamoja na kuwa karibu na msichana mrembo kama yeye, na kumuonyesha upendo, lakini hakuonana kuwa na tamaa ya mwili. Badala yake alikuwa akimjali na kumpa upendo bila kuhusisha na mambo mengine.

Kitendo hicho kilimfanya Bishada kujiona na thamani. Hakujiona ni chombo cha kumfurahisha mtu. Bali ni binadamu ambaye anahitaji

> **Bishada aliangua kicheko, akaichukua na kuipeleka kwa mama yake. Mama aliipokea kwa mikono miwili. Alijua kabisa kuwa hiyo itakuwa ni barua ya mwisho.**

faraja, kupendwa, kuthaminiwa na kujaliwa.

Hilo lilimfanya kuanza taratibu kumpenda Denny. Na si kumpenda kwaida tu, kumpenda ndano ya moyo wake. Ni yeye ndiye aliyekuwa akianza kumgusa wanapocheka na kufurahi. Alijisikia vizuri sana anapogusa ngozi na Denny. Kuna kitu ambacho hakuwahi kukihisi kabla.

Ni mapenzi. Sasa alitaka mchumba. Na si mwingine ila ni Denny.

Kwa upande wake Denny, pamoja na kuwa alikuwa Dar na kukutana na wanawake wengi, lakini alishangazwa na uzuri wa msichana huyo ambaye anaishi kijijini.

Si kwamba alitakiwa awe anaishi mjini kwa jinsi alivyo, lakini aliwazidi uzuri wasichana wengi mjini ambao wametumia gharama kubwa kwa kujipamba saluni na kuvaa nguo za gharama.

Alishangazwa na uzuri wa Bishara licha ya kwamba hakuwa anakwenda saluni, bila ya kuwa na nguo za gharama. Ni kama dhahabu iliyokuwa chini ya mchana au matope.

Aliona akiipeleka mjini itazidi kung'aa zaidi "Hivi huyu mtoto akifika mjini, aende saluni kuvaa nguo za gharama itakuwaje?" Alijiuliza.

Kingine ni ubichi ya msichana huyo. Alikuwa na miaka 23 tu. Alitokea kumpenda tangu siku ile aliupomuokoa kwa jamaa aliyetaka kumbaka. Lakini hakutaka kuchukua pupa wala haraka. Alijua muda utafika Na kweli ulifika. Wote wawili walijikuta wako kwenye lengo moja.

Kila mmoja alimueleza mwezake kinachomsibu moyoni. Kila mmoja akimfungukia mwenzake.

Denny aliandika barua na kumwambia kwa sababu hatokuwa na mshenga, basi yeye mwenyewe Bishada ndiyo awe mshenga.

Bishada aliangua kicheko, akaichukua na kuipeleka kwa mama yake. Mama aliipokea kwa mikono miwili. Alijua kabisa kuwa hiyo itakuwa ni barua ya mwisho. Kwa sababu anayekataa kila barua inayoletwa hapo, ndiye aliyeleta barua hiyo.

Baada ya taratibu zote kufanyika, barua ile ikapelekwa kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji.

Ilipelekwa kwa sababu maalum. Ni kwa sababu ilikuwa bado siku mbili tu ili wafurushwe kwenye kijiji hicho kama binti yao Bishada atakuwa hajaolewa au kuchumbiwa.

Angalau sasa mzee Ngoma na mkewe Fatuma walianza kuona mwanga. Nao ni wa kubaki kwenye kijiji hicho na pia binti yao sasa kupata mume.

**ITANEDELEA JUMAMOSI**

# TITE AFURAHIA NEYMAR KUMKARIBIA PELE




**BRASILIA,** Brazil

NEYMAR alifunga kwa mara ya nne mfululizo kwenye mechi za kimataifa na kubakia na mabao tisa kufikia rekodi ya ufungaji ya wakati wote ya Pele na kocha Tite amesema hakuna kikwazo kwa nyota wake huyo.

Neymar alifunga bao moja na kutoa mchango kwenye mengine matatu wakati Brazil ambao ni mabingwa watetezi wa Copa America wakiifumua Peru 4-0 katika mchezo wao wa pili wa michuano hiyo, juzi.

Neymar alifikisha mabao 68 kwa kikosi cha Brazil, akiwa nyuma ya gwiji wa Selecao hao, Pele mwenye mabao 77.

Tangu alipoanza kuichezea Brazil mwaka 2010, Neymar amefunga mabao zaidi ya 49 yakiwa mengi zaidi kuliko mchezaji mwingine yoyote kwenye kikosi hicho kwa kipindi hicho.

"Sijui wapi Neymar anaweza kufikia," alisema Tite wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Katika suala la mbinu na uwezo, kwa hakika natumaini mara zote atakuwa na afya njema na hatapata majeruhi."

Tangu Tite alipochukua mikoba ya kuinoa Brazil mwaka 2016, Selecao hao wamefunga mabao 37 katika mechi 56.

# Alves aitwa kikosi cha Brazil cha Olimpiki

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

DANI Alves amejumuishwa huku Neymar akiachwa kwenye kikosi cha Brazil cha wachezaji 18 kitakachokwenda kutetea medali ya dhahabu kwenye michezo ya Olimpiki 2020 jijini Tokyo.

Kocha wa Brazil wa kikosi hicho cha Olimpiki, Andre Jardine, alithibitisha kikosi chake Alhamisi, huku mlinzi wa pembeni wa Sao Paulo mwenye umri wa miaka 38 Alves akiwa mmoja wa wachezaji watatu wenye umri mkubwa, pamoja na nyota wa Sevilla, Diego Carlos na golikipa wa Athletico PR, Santos.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona, Juventus na Paris Saint-Germain, Alves, ambaye amecheza mechi 118 za kimataifa, alipangwa kuwa sehemu ya kikosi cha Brazil kwenye michuano ya Copa America, lakini ameikosa kutokana na majeruhi ya goti na badala yake atakuwa katika kikosi cha Olimpiki.

Nyota wa PSG, Neymar, ameachwa kwenye michezo hiyo, licha hapo mwanzo kuonesha nia ya kuwapo kwenye michezo hiyo ya Tokyo.

Kiungo wa Aston Villa, Douglas Luiz, nyota wa Lyon, Bruno Guimaraes na mkali wa Flamengo, Pedro pia wamejumuishwa kwenye kikosi cha Brazil.

Brazil walishinda medali ya dhahabu kwenye michezo ya Olimpiki iliyofanyika mwaka 2016 jijini Rio de Janeiro, huku Neymar akifunga penalti ya ushindi wakati wakishinda 5-4 dhidi ya Ujerumani.

Brazil ipo kundi D pamoja na Ujerumani, Ivory Coast na Saudi Arabia.

Brazil itafungua dimba dhidi ya Ujerumani mjini Yokohama Julai 22.






# Villa yamsajili Young

**LONDON,** England

ASTON Villa imemsajili Ashley Young kwa uhamisho huru baada ya kuondoka kule Inter Milan.

Young amekubali kusaini mkataba wa mwaka mmoja pale Villa Park, muongo mmoja baada ya kuondoka Manchester United.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa England alitumia miaka minne na nusu kucheza pale Villa hapo awali na alicheza mechi 190 katika mashindano yote.

Villa ilithibitisha kuwasili kwa Young katika tovuti yake Alhamisi na mchezaji huyo alisema: "Najisikia vizuri sana kurudi tena, naona kama vile sikuondoka.

"Kwa hakika nimefurahia kurudi, kuona baadhi ya sura za zamani uwanjani, kuona vitu nilivyoviacha na timu iliyokua zaidi.

"Unaweza kuona namna klabu ilivyokuwa tangu nilivyoondoka na nipo tayari kuendelea tena kufanya kazi hapa."

Young alicheza mechi 34 kwa Inter Milan ambao walishinda taji la Ligi Kuu msimu wa 2020-21 na alifunga bao moja.

Kabla ya kujiunga na Inter, Young alishinda taji la Ligi Kuu England, FA, EFL na Ligi ya Europa akiwa na United.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 ni usajili wa pili kwa Villa baada ya kumpata Emiliano Buendia kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo wiki iliyopita.

HABARI MICHEZO

# Eriksen kuwekewa kifaa kwenye moyo

**COPENHAGEN.** Denmark

NYOTA wa Denmark, Christian Eriksen, anatarajiwa kuwekewa kifaa maalumu cha moyo, baada ya kuanguka kwake uwanjani wakati wa mchezo wa Euro 2020.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 29 alipatwa na mshituko wa moyo na kudondoka uwanjani Jumamosi iliyopita katika mchezo ambao Denmark ililala kwa bao 1-0 dhidi ya Finland.

Daktari wa timu ya taifa ya Denmark, Morten Boesen, amesema kifaa hicho kinachojulikana kitaalamu kwa kifupi 'ICD', ni muhimu hasa wakati huu ambapo moyo wa mchezaji huyo una mapigo yasiyo ya kawaida.

Hadi sasa Eriksen bado yuko hospitalini akiendelea na tiba, ingawa mwenyewe anasema anaendelea vizuri kwa sasa.

Mlinzi wa Uholanzi, Daley Blind, aliwahi kupata tatizo la moyo mwaka 2019, lakini alirejea uwanjani Februari 2020 baada ya kuwekewa kifaa hicho cha ICD.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 yuko na timu yake hiyo ya taifa kwenye Euro 2020, ambapo alicheza kwenye mchezo wa kufungua dimba, Uholanzi ikiizaba Ukraine 3-2.





# DE BOER ATAKA UHOLANZI KUIMARIKA

**AMSTERDAM,** Uholanzi

FRANK de Boer anaitaka Uholanzi "kukua" kwenye Euro 2020 baada ya kuifunga Austria 2-0 na kutinga hatua ya mtoano ya timu 16 akiwa mshindi wa kundi C.

Bao la penalti la kipindi cha kwanza kutoka kwa Memphis Depay na lile la Denzel Dumfries lilitosha kuiwezesha Uholanzi kushinda mchezo wake wa pili wa mashindano hayo pale kwenye dimba la Johan Cruijff ArenA, juzi Alhamis.

Uholanzi wangeweza kupata mabao mengi kwenye mchezo huo, kama Depay angekuwa makini na kutopoteza nafasi alizopata kipindi cha kwanza.

Na sasa kocha wa Uholanzi, De Boer anataka kuona kikosi chake kikiongeza ubora na kuwa timu ya kwanza ya Oranje kufunga angalau mabao mawili katika mechi tisa mfululizo tangu mwaka 1935.

"Unatakiwa kukua kwenye mashindano na hasa ukifikiria kwamba mnacheza kama timu kwa pamoja," alisema De Boer.

"Vijana watakuwa na majadiliano namna gani wanaweza kuimarika zaidi, namna ya kukua kwenye mashindano.

# *De Bruyne analeta tofauti - Martinez*

**COPENHAGEN,** Denmark

KIWANGO cha Kevin De Bruyne kwenye mchezo ambao Ubelgiji ilishinda 2-1 dhidi ya Denmark kilisifiwa kama "cha kufurahisha sana" na kocha, Roberto Martinez.

Baada ya kuukosa mchezo wa kwanza wa Ubelgiji wa ushindi wa 3-0 dhidi ya Russia kutokana na kuumia pua katika fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya, De Bruyne alirudi na kufunga hapa Copenhagen, juzi Alhamisi.

Yussuf Poulsen alifunga dakika ya pili kwenye mchezo huo na kuiweka mbele Denmark, lakini Thorgan Hazard alisawazisha kwa Ubelgiji dakika tisa baada ya kipindi cha pili baada ya kucheza vizuri na De Bruyne.


Halafu De Bruyne akafunga la ushindi zikiwa zimesalia dakika 20 mpira kumalizika, kwa shuti kali eneo la penalti.

Uwepo wa De Bruyne mwanzoni mwa kipindi cha pili uliimarisha timu na Martinez amesema mabadiliko yaliongeza ubora kwa timu.

"Kamwe huwezi kuwa na shaka na kipaji cha De Bruyne," alisema Martinez akiwaambia waandishi wa habari.

"Bila shaka ni kazi kubwa ilifanyika kipindi cha pili na kilileta tofauti kwenye mchezo wote.

"Sio tu kuhusu kipaji, pia ni namba unavyoweza kujua njia ya kucheza na ndivyo alivyofanya De Bruyne."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAKIMI SASA MAMBO YAMETIKI CHELSEA

●●● Ofa ya pauni mil 40 yatolewa, PSG nao watia mguu wao...

**PARISA,** Ufaansa

CHELSEA inaonekana kushinda kwenye mbio za kuwania saini ya mlinzi wa Inter Milan, Achraf Hakimi, baada ya kufikia makubaliano ya mdomo kujiunga na mabingwa hao wa Ulaya.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa Calcio mjini Pillole, Ekrem Konur, makubaliano ya mdomo kati ya Hakimi na Chelsea yameshafikiwa na pande zote mbili kukubaliana.

Mabingwa hao wa Ulaya, Chelsea wamekuwa wakimbana na miamba wa Ufaransa, Paris Saint-Germain kwenye mbio za kuwania saini ya Hakimi.

**Hakimi mchezaji wa kimataifa wa Morocco mwenye umri wa miaka 22, aliisaidia Inter kutwaa taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa mara ya kwanza msimu huu baada ya kipindi cha miaka 10.**

Beki huyo wa pembeni wa zamani wa Borussia Dortmund na Real Madrid nyota yake kwa sasa imekuwa iking'aa zaidi baada ya kuonesha kiwango cha kuvutia kule Inter.

Mwandishi Konur amedai kwamba, Inter wanataka kiasi cha pauni milioni 43 ili kumuachia mchezaji huyo na wanamtaka mlinzi wa pembeni, Marcos Alonso kutoka Chelsea kuwa sehemu ya dili hilo.

Lakini Footmercato limeripoti kwamba, PSG watarudi tena mezani kwa Inter kwa ajili ya kutoa ofa nyingine ya kumsajili Hakimi.

Na kwa mujibu wa ripoti hiyo, PSG wapo tayari kutoa kiasi cha euro milioni 70 ili kuapata saini ya Hakimi.

## ZISIKUPITE

### EVERTON KUMSAJILI COADY

EVERTON wanataka kumsajili nyota wa Wolves na England, Conor Coady, 8. ***(Football Insider)***

### MAN YAJITOSA KWA VARANE

KLABU ya Manchester United wamepata ombi la kufungua ofa ya pauni milioni 50 kwa beki wa Real Madrid na Ufaransa, Raphael Varane, lakini Real wanataka pauni milioni 80 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Manchester Evening News)***

### VARANE NA MKATABA MPYA

KUONDOKA kwa Sergio Ramos kutoka Real Madrid kunaweza kudhoofisha mipango ya Manchester United ya kumsajili Raphael Varane, baada ya wababe hao wa Hispania kufungua mazungumzo ya mkataba mpya na beki huyo wa kati. ***(Times)***

### PSG YAKOMAA NA HAKIMI

KLABU ya PSG inajiandaa kuweka mezani ombi la pili la kumsajili Achraf Hakimi la euro milioni 7. ***(Footmercato)***

### ROMA YAMTAKA LUIZ

KLABU ya AS Roma itajaribu kumsajili kiungo wa Aston Villa na Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 23, ikiwa watashindwa kumpata kiungo wa Arsenal na Uswizi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 28. ***(Gazzetta dello Sport)***

### PALACE YAMUWANIA FAVRE

CRYSTAL Palace wamefanya mawasiliano na mwakilishi wa kocha wa zamani wa Borussia Dortmund, Lucien Favre wakati wanaendelea na utafutaji wa kocha mpya. ***(Guardian)***

### LOKONGA AWANIWA ARSENAL

ALBERT Lokonga mwenye umri wa miaka 21 wa klabu ya Anderlecht na kipa wa Sheffield United na England, Aaron Ramsdale mwenye miaka 23, ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na Arsenal, wakati kocha Mikel Arteta anataka kurekebisha kikosi chake. Kiungo wa kati wa Ubelgiji, Lokonga anasemekana kuwa na thamani ya pauni milioni 17.5 ***(Goal)***

### TIELEMANS KUSAINI

LEICESTER City ina matumaini kwamba, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24, atasaini mkataba mpya klabu hiyo, huku kukiwa na uvumi kuhusu hatima yake. Kiungo huyo wa Ubelgiji amekuwa akihusishwa na Manchester United na Liverpool. ***(Leicester Mercury)***

### PATSON ATAKIWA LEICESTER

KLABU ya Leicester City imeongeza nia yake ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa RB Salzburg na Zambia, Patson Daka mwenye umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

### LINGARD ATAKA KUJUA HATIMA

KIUNGO Jesse Lingard, 28 anayecheza kwa mkopo kule West Ham, anatarajiwa kufanya mazungumzo na Manchester United juu ya hatma yake atakaporudi kwa mazoezi ya kujiandaa kwa msimu ujao. ***(Star)***

HABARI MICHEZO

## Zimamoto yajipanga kwa msimu ujao

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya Zimamoto, Mohmed Ali Hilali "Teddy" amesema baada ya kutolewa katika michuano ya Kombe la Shirikisho la soka Zanziba, ZFF, sasa anaijenga timu hiyo kwaajili ya kujiandaa na msimu ujao.

Zimamoto imeondolewa katika kombe hilo na timu ya Kilimani City kwa kufungwa 1-0, mchezo uliopigwa katika uwanja wa Amaan, juzi.

Akizungumza na gazeti hili, kocha huyo alisema kuondolewa katika michuano hiyo hivi sasa kunamfanya ajikite katika kuboresha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao wa ligi kuu.

Alisema msimu uliopita timu hiyo katika mzunguko wa kwanza haukufanya vizuri sana licha ya kumaliza nafasi ya pili katika msimamo wa ligi kuu ya Zanzibar.

Alisema kutokana na ugumu wa ligi yenyewe pamoja na uchache wa timu za ligi hiyo, msimu mpya anatarajia kushuka na kikosi ambacho kitaleta mafanikio.

"Baada ya kuukosa ubingwa, matumaini yetu tulihamishia katika kombe la FA nalo pia tumelikosa, hivyo tunajiandaa na maandalizi ya mapema kuelekea msimu mpya, najua utakuwa msimu wa ushindani," alisema.

## Ngoma za asili, kwaya kurindima Agosti 8

**Na Sabato Kasika**

MASHINDANO ya ngoma za asili na kwaya kwa mwaka 2021, katika Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, yanatarajia kufanyika Agosti 8, mwaka huu, katika Kijiji cha Suguti jimboni humo.

Akizungumza na gazeti hili, msaidizi wa mbunge wa jimbo hilo, Fedison Masawa, alisema, ofisi wa mbunge Prof. Sospeter Muhongo ndiyo ambayo huratibu mashindano hayo kila mwaka.

"Mashindano haya huandaliwa kila mwaka na ofisi ya mbunge, kwa lengo la kufufua ngoma za asili na kwaya, lakini pia kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wakazi wa jimbo letu," alisema Masawa.

Msaidizi huyo wa mbunge alisema, kila kata itatoa kikundi kimoja cha ngoma za asili na kingine cha kwaya, na kwamba zawadi zitatolea na Prof. Muhongo kwa mshindi wa kwanza hadi wa tatu.

Aidha, Masawa alifafanua kuwa jimbo hilo lina kata 21 na kwamba kila kata itakuwa na vikundi viwili, vitakavyoshiriki katika mashindano hayo ambayo pia yanalenga kukuza na kuendeleza vipaji.

"Kwa sasa hatuwezi kutaja aina ya zawadi kwa washindi, lakini uhakika ni kwamba zitakuwepo na zitatolewa na mbunge mwenyewe kwa vikundi ambavyo vitaibuka na ushindi," alisema.

# FEI TOTO: HATUJAKATA TAMAA NA UBINGWA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufunga mabao mawili, akiibeba timu yake ya Yanga kupata ushindi wa 3-2 dhidi ya Ruvu Shooting juzi Alhamisi, kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', amesema kuwa bado hawajakata tamaa ya kuupata ubingwa wa Ligi Kuu.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa mara baada ya mechi hiyo, Feitoto alisema kuwa wanachokifanya sasa ni kuhakikisha kuwa wanashinda kila mchezo kwani kwenye soka lolote linaweza kutokea na wao kutwaa ubingwa.

"Hatujakata tamaa. Ubingwa bado upo kama tunashinda mechi zilizobaki, halafu tutaangalia huko mbele kwa sababu huu ni mpira na chochote kinaweza kutokea," alisema.

**Kiungo huyo alieleza kufurahishwa kuwa kwenye kiwango bora kwa siku za karibuni, kwani hata kwenye mechi ya Taifa Stars dhidi ya Malawi, aliibuka kuwa mchezaji bora wa mechi.**

"Hakuna siri ya yote haya, zaidi ya kujituma, kufanya mazoezi kwa bidii na kusikiliza walimu nini wanakuelekeza na nini ufanye uwanjani," alisema.

Fei Toto alisema kuruhusu mabao mawili kwenye wavu wao kulitokana na wao wenyewe kufanya makosa ndiyo maana wakaadhibiwa.

Kwa matokeo hayo, Yanga imefikisha pointi 64, tatu nyuma ya vinara Simba yenye pointi 67, lakini ikiwa imecheza mechi tatu zaidi yao.

Ruvu Shooting ina pointi 37 na ipo kwenye nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi..




Wachezaji wa timu ya wanawake ya mpira wa Kikapu wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mbio Lake Victoria kufanyika kesho*

**Na Sabato Kasika**

WANARIADHA sita waliopo katika kambi ya timu ya taifa ya Tanzania watashiriki mbio za Lake Victoria zitakazofanyika jijini Mwanza kesho Jumapili, imeelezwa.

Mbali na wanariadha hao wa timu ya taifa, waandaaji wa mbio hizo ambazo ni za kwanza kufanyika, tayari wameshasajili washiriki 250 katika mbio za kilometa 250, 150 kwa kilometa 150 na 160 kwa wale wa mbio za kilometa 21.

Mratibu wa mbio hizo, Frank Tendwa akizungumza kwa njia ya simu kutoka Mwanza jana alisema kuwa lengo lao ni kuandikisha washiriki 250 katika mbio za kilometa 21 na kupata jumla ya washiriki 650 katika mbio za mwaka huu.

"Tumeshafunga usajili wa mbio za kilometa tano na 10 baada ya watu 250 na 150 kujiandikisha katika mbio hizo na zile za kilometa 21 tayari tumeandikisha 160, bado 250 katika mbio hizo ili ifikie 650 ambao ndio lengo letu, "alisema Tendwa.

Naye Nelson Mrashani ambaye amekuwa akiitafutia wadhamini timu ya taifa ya riadha kwa ajili ya kushiriki mbio mbalimbali za majaribio alithibitisha jana kuwa wanariadha wa taifa watashiriki mbio hizo.

Mrashani aliwataja wanariadha hao ambao wanajiandaa kwa Michezo ya Jumuiya ya Madola na Afrika kuwa ni pamoja na Emmanuel Giniki, Wambura Lameck na Faraja Damas watakaoshiriki kilometa 10, Joseph Gisemo, Inyasi Sulle na Alyoce Simbu watashiriki kilometa 21.

Mrashani aliyefanikisha safari ya wanariadha wa taifa kushiriki katika mbio za Mbeya Tulia 2021 na zile za Bima jijini Mbeya na Dar es Salaam kwa udhamini wa Kampuni ya Silent Ocean, alisema ataendelea kuisaidia timu hiyo.

Hivi karibuni timu hiyo ya taifa ilipatiwa chakula na vifaa vingine vyenye thamani ya zaidi ya Sh milioni 3 kutoka Silent Ocean kwa ajili ya kambi yao iliyopo katika hosteli za Chuo Kikuu cha Sokoine Olimotonyi kwa ajili ya maandalizi ya Michezo ya Olimpiki na mingine ya kimataifa.

Wanariadha wa taifa walitamba katika mbio za Tulia na zile za Bima na sasa wanatarajia kufanya vizuri katika Lake Victoria Marathon 2021.

# Michezo

Jumamosi Juni 19, 2021

Nipashe




Hakimi mambo yametiki Chelsea

UKURASA 22



Memphis Depay wa Uholanzi (kushoto), akipiga mpira mbele ya Christoph Baumgartner wa Austria, wakati wa mchezo wa michuano ya Euro 2020 baina ya timu hizo, kwenye uwanja wa Johan Cruijff Arena jijini Amsterdam juzi Alhamisi. Uholanzi ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# KIPA METACHA ASIMAMISHWA

## ●●● Uongozi wa Yanga wakerwa kitendo cha kuwatusi mashabiki, mwenyewe aomba...

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Yanga umemsimamisha kipa wake, Metacha Mnata kutokana na utovu wa nidhamu, Kocha mkuu wa timu hiyo, Nesreddine Nabi, amesema kitendo alichokifanya ilikuwa ni jazba na hasira baada ya kuchukizwa na mashabiki wa Yanga kumzomea.

**Yanga imemsimamisha kipa wake huyo namba moja, Mechata kwa muda usiojulikana kutokana na utovu wa nidhamu.**

Mashabiki wa Yanga walikerwa na kitendo cha Mnata kuruhusu mabao mawili rahisi timu ikishinda 3-2 dhidi ya Ruvu Shooting katika mchezo wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara uliofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jijini Dar es Salaam, juzi.

Na wakati anatolewa uwanjani kwa msaada wa Polisi kumuepusha na mikono ya mashabiki wenye hasira waliokuwa wanamtolewa maneno makali na kumtupia chupa, kipa huyo akawaonyesha ishara ya kuwatusi.

Uongozi wa Yanga ulitoa taarifa kwamba umesikitika na kitendo kisichokuwa cha kiungwana alichokifanya Metacha na anasimamishwa hadi hapo suala lake litakapofikishwa mbele ya kamati ya nidhamu ya klabu hiyo.

"Tunaomba radhi kwa wanachama, wapenzi na mashabiki na wadau wa michezo kwa kitendo hicho alichokifanya kipa wetu uongozi utachukuwa hatua ya kumpeleka kwenye kamati ya Nidhamu ya klabu kwa hatua zaidi," alisema taarifa ya Klabu hiyo.

Nabi alisema hakupendezwa na kitendo alichokifanya, lakini pamoja na mashabiki wa Yanga kumzomea mchezaji huyo hawakuwa sahihi hata akiwa amefanya makosa uwanjani, ana imani wangetumia njia nyingine.

Wakati huo huo, Mnata mwenyewe jana aliomba kupitia ukurasa wake rasmi wa Instagram akisema: "Kwa niaba ya familia yangu, Management yangu na mimi mwenyewe napenda kuchukua fursa hii kuomba msamaha kwa viongozi wa klabu yangu ya Yanga SC, wachezaji wenzangu, benchi la ufundi, mashabiki wa Klabu ya Yanga, Mamlaka za soka nchini na wadau wote soka ambao wamekwazika kwa kwa kitendo nilichokifanya jana.

"Nikiri hakikuwa kitendo cha kiungwana hivyo najutia makosa niliyoyafanya. Mimi kama mchezaji wa Yanga na Timu ya Taifa napaswa kuwa mfano mzuri siku zote mbele za watoto na wanaotamani kuwa kama mimi na watu ambao aidha walikuwepo uwanjani au waliona mechi kupitia Televisheni majumbani kwao. Natambua mchango na umuhimu wa mashabiki kwangu binafsi na kwa Klabu, hivyo kitendo kile hakikupaswa kutokea."

## Simba kusaka pointi za ubingwa

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, leo watakuwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza kusaka pointi tatu muhimu ambazo zitawasogeza karibu na ubingwa, dhidi ya Polisi Tanzania.

Simba inahitaji angalau ushindi kwenye mechi tatu kati ya saba ilizobaki nazo ili kutawazwa mabingwa kwa mara ya nne mfululizo.

Polisi Tanzania ambayo ndiyo mwenyeji kwenye mechi hiyo kwa kupeleka mechi yao kwenye uwanja huo badala ya Ushirika Moshi, itakuwa na kazi kubwa ya kuizuia Simba ambayo imekuwa ina mwendelezo mzuri wa ushindi.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema kuwa anajua mechi itakuwa ngumu kwa sababu Polisi Tanzania wana tabia ya kuwakamia mno, lakini wana imani kuwa wataibuka na ushindi.

"Mechi yetu shidi ya Polisi Tanzania siku zote haijawahi kuwa nyepesi. Ni kweli tumekuwa tukishinda mechi zote, mbili Dar es Salaam na moja Moshi, lakini ukiangalia hatukushinda kwa urahisi," alisema Matola.

Alisema wamekwenda Mwanza na kikosi kiko kamili, ingawa kinawakosa wachezaji wawili tu ambao ni Clatous Chama ambaye bado yupo kwenye mapumziko ya kufiwa na mkewe na Ibrahim Ajibu ambaye ni mgonjwa.

Na kwa upande wa nahodha wa Polisi Tanzania, Pato Ngonyani, amesema kuwa kwa walivyojipanga, wana imani kuwa wanaweza kupata matokeo kwenye mechi ya leo dhidi ya Simba, ingawa aliongeza kuwa mechi itakuwa ngumu kwa sababu Simba ina wachezaji wazoefu.

## Yanga vs Mtibwa fainali U20 leo

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi ya Vijana chini ya umri wa miaka 20 (U20), Mtibwa Sugar, watashuka dimbani leo saa 1:00 usiku kucheza na Yanga katika fainali ya michuano hiyo kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi Dar es Salaam.

Mtibwa imetinga fainali hiyo baada ya kuifunga Simba 3-1, huku Yanga ikiifunga Azam kwa changamoto ya mikwaju ya penati 6-5 baada ya kukamilika kwa dakika 120 kwa sare ya bao 1-1.

Mtibwa wanawania kulibeba kombe hilo kwa mara ya tatu mfululizo, wakianza msimu wa 2018 fainali zilizofanyika jijini Dodoma na 2019 kufanyika jijini Dar es Salaam na mwaka jana ilishindikana kufanyika kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Yanga hiyo inakuwa ni mara ya pili kucheza fainali, mara ya mwisho walicheza mwaka 2013.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >